# KATIBA

## YA

## JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA

**KIMETAYARISHWA NA**
**KAMATI KUU YA JUMUIYA**

**TOLEO LA PILI JUMADAL- AKHAR 1427 H**
**JULAI 2006 M**

# YALIYOMO

Ukurasa

**I. UTANGULIZI........................... 5**

A. CHANZO NA KUANDIKISHWA KWA JUMUIYA.....5
B. KAZI ZA JUMUIYA NA MAFANIKIO YAKE ...........8
C. HALI YA JUMUIYA NA MATATIZO YAKE..............10
D. UENDESHAJI .....................................12
E. UFAFANUZI WA KIDINI.......................16
1. KIINI CHA DINI YA KIISLAMU........... 16
2. SHARIA NA KAZI ZAKE..................... 17
3. TWARIQA NA KAZI ZAKE............... 21
4. MSINGI WA TWARIQA..................25
5. IJAZA........................................... 28
6. MALEZI YA TWARIQA...................31
7. ZAWIYA.......................................35
8. MADHEHEBU ZA TWARIQA........... 40
9. TWARIQATUL QADIRIYA.............. 42
10. MWISHO.................................... 45

**II.**

**KATIBA ..........................47**

**SEHEMU YA KWANZA** .........................47
UTAMBULISHO NA UWEZO WA JUMUIYA..... 47
A. JINA .........................................47
B. OFISI ZA JUMUIYA .......................47
(i) MAKAO MAKUU .....................47
(ii) OFISI NDOGO ........................48
C. AKAUNTI ZA BENKI .................... 48
D. UWEZO WA JUMUIYA ................. 50
E. UANA JUMUIYA ........................50

**SEHEMU YA PIL ................................. 51**

MADHUMUNI................................... 51
A. MADHUMUNI MAKUBWA .............. 51
B. ELIMU NA IBADA .......................... 52
C. AFYA ........................................... 53
D. KILIM ........................................... 54
E. BIASHARA ........................................ 54
F. HUDUMA NYINGINEZO ...................... 54

**SEHEMU YA TATU** ..................................... 56
A.VIONGOZI WA JUMUIYA ........................ 56
1. MLEZI WA JUMUIYA ....................... .. 56
2. MWENYEKITI WA JUMUIYA ................. 58
3. MANAIBU WENYEVITI ......................... 59
4. KATIBU MTENDAJI .............................60
5. MANAIBU MAKATIBU WATENDAJI ...... 61
6. WAKUU WA IDARA ........................... 62
7. VIONGOZI WA VITUO .................. 63
8. VIONGOZI WA MAZAWIYA ........... 65
B. VIKAO VYA JUMUIYA ......................68
1. MKUTANO MKUU WA JUMUIYA ......68
2. KAMATI YA MASHEIKH .................. 70
3. BARAZA LA WADHAMINI ............... 72
4. KAMATI KUU ............................... 74
5. SEKRETARIETI ............................ 76
6. KAMATI ZA UTENDAJI ZA OFISI NDOGO... 79

**SEHEMU YA NNE** ................................ **81**
MENGINEYO ...................... ........... 81
A. ALAMA YA JUMUIYA ................... 81
B. MUHURI ....................................... 81
C. VITAMBULISHO ............................ 82

D. KUACHA UONGOZI ……………….…. 82
E. KUHAMA ………………………….…. 83
F. UHALALI WA VIKAO VYA JUMUIYA (QUORUM) …………………………… 83
G. UTATUZI WA MATATIZO ……………. 83
H. KUSIMAMISHWA UONGOZI ……….. 84
I. MALIPO ………………………………. 84
J. MAREKEBISHO YA KATIBA ………….. 85

**SEHEMU YA TANO ………………………….. 86**

A. UTHIBITISHO (CERTIFICATION) .……… 86
B. VIAMBATANISHO ……………………… 87
1. KIAMBATANISHO "A" ……………… 87
SILSILAH YA TWARIQATUL QADIRIYA UWEISIYYAH ……………………….87
2. KIAMBATANISHO "B" ………………. 89
MAOMBI YA KUJIUNGA NA JUMUIYA 89
3. KIAMBATANISHO "C" ………………….92
KALENDA YA HADHARA ZA KAWAIDA KATIKA MWAKA ………………… 92
4. KIAMBATANISHO "D" ……………..…. 99
MUUNDO WA SEKRETARIETI ………… 99
5. KIAMBATANISHO "E" ………………. 100
MUUNDO WA JUMUIYA …………. 100

# I. UTANGULIZI

## A. CHANZO NA KUANDIKISHWA KWA JUMUIYA

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutupa uzima na afya pamoja na kutujaalia uwezo wa kupata Jumuiya yetu hii, JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA. Ili kudumisha umoja wetu KI-DINI katika misingi imara zaidi, tumeamua kuunda Jumuiya ya kutuwezesha kuendeleza umoja wetu kihalali kwa faida zetu, vizazi vyetu vya sasa na vya baadaye na Waislamu wote.

Katika zama hizi tulizonazo, hali halisi ya Waislamu katika elimu ya Dini, Imani, ucha Mungu, na uongozi wa Dini ni duni sana. Kwa hiyo, sisi wafuasi wa Twariqa ya Qadiriya hapa Tanzania tumeamua kujitambulisha rasmi kwa Serikali zetu na kwa Waislamu wenzetu kote nchini. Ili kufanikisha nia hiyo, na kufuatana na sheria ya nchi yetu, tumejiandikisha kama Jumuiya rasmi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kutambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mategemeo yetu ni kwamba, chombo hiki kitakuza na kuimarisha mapenzi na mashirikiano mema baina yetu na Waislamu wengine popote walipo. Lengo letu Waislamu sote ni moja: ***kufuata kumjua Mola wetu na kupata***

***radhi zake.*** Jumuiya yetu hii ni ya KI-DINI. Hivyo tumetengeneza Katiba hii katika misingi ya maadili ya Qur'ani na Sunna za Bwana Mtume Muhammad (SAW).

Juhudi za kuiandikisha Jumuiya yetu hii zilianza katika mwaka 1980. Kwa bahati mbaya hatukufanikiwa wakati huo. Lakini Mwenyezi Mungu (SW) amejaalia, kwa bidii na juhudi za ndugu zetu wa Arusha, tumeweza kuandikishwa. Tulianza kwa kuandikisha udhamini kwa jina la MASJID ZAWIYA EL-QADIRIYA AND ISLAMIC CENTRE mnamo tarehe 7/1/1988 na kutangazwa katika gazeti rasmi la Serikali. Jitihada ziliendelea kufanywa na ilipofika mwaka 1990, tukafanikiwa kukiandikisha chombo hiki Wizara ya Mambo ya Ndani na kupewa Hati ya kuandikishwa Nambari S.O.7168 ya tarehe 2/11/90.

Katika Mkutano Mkuu wa kwanza uliofanyika tarehe 26/9/91 hadi 29/9/91 huko Arusha, wajumbe katika kujadili Katiba, walikubaliana kubadili jina ili chombo hiki kitambulikane kuwa ni cha nchi nzima. Jina jipya lililokubaliwa lilikuwa JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA (yaani Jumuiya ya Mazawiya ya Twariqa ya Qadiriya hapa Tanzania). Tarehe 10/4/1992, Wizara ya Mambo ya Ndani ilitoa Hati nyingine ya uandikishaji nambari S.O.7168 kwa jina jipya.

Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Wadhamini nayo tarehe 9/11/1992 ilitoa Hati mpya kwa jina jipya na kutangaza katika gazeti la Serikali la tarehe 27/11/1992 ukurasa 937, tangazo nambari 947.

Misingi na chanzo cha Jumuiya hii inatokana na Twariqa. Kwa miaka mingi sasa tangu Uislamu uingie katika nchi yetu (Al-Hamdulillah) mafunzo ya Twariqa yamekuwa yakitolewa na Mashekhe mbalimbali na taratibu zake za Ibada zimekuwa zikifuatwa. Lakini kutokana na hali ya ulimwengu ulivyo na nyoyo kumili katika ulimwengu tukaonelea iko haja kuzidi kukumbushana katika Dini yetu. Hivyo, katika mazingira ya aina hii, imebidi tuzidishe bidii katika kuzisafisha nafsi zetu kwa kushikamana na Twariqa.

## B. KAZI YA JUMUIYA NA MAFANIKIO YAKE

Hadi hivi sasa, jitihada zetu nyingi zimeelekea katika kujenga na kusimamia Misikiti, kujenga na kuendesha vyuo vya kusomeshea Qur'ani, kutoa malezi na mafunzo ya Ki-Twariqa, na kuendesha taratibu nzuri za Ibada kama zilivyopokelewa kutoka kwa BWANA MTUME MUHAMMAD (S.A.W). Al-Hamdulillahi sasa tunayo Misikiti zaidi ya mia mbili (200) na vyuo vya Qur'ani visivyopungua mia nne (400) katika

mikoa mbali mbali ya Tanzania Bara, Unguja na Pemba.

Wazazi wengi kutoka sehemu mbali mbali za Tanzania wamekuwa wakituletea watoto wao ili tuwasomeshe Qur'ani na tuwafunze na kuwapatia malezi ya Ki-Tasawwuf/Ki-Twariqa, kwa maneno mengine, tuwalee katika misingi ya Ucha-Mungu. Baada ya kukaa nao kwa miaka kadhaa, kwa idhinii ya wazazi wao, tumekuwa tukiwapeleka baadhi ya vijana hawa sehemu mbali mbali kwenye Misikiti na vyuo vyetu ili wakasaidie kusomesha na kuongoza Ibada chini ya usimamizi wa wazee wa sehemu hizo. Matumizi ya kuendesha maisha ya baadhi ya vijana hawa yamekuwa yakikabiliwa kwa kiwango kikubwa na wenyeji wao ambao, aghalabu huwa ndio waliotuomba tuwapelekee Walimu wa kuwasomeshea watoto wao.

Wakati mwingine, kutokana na hali duni ya wenyeji wao, imebidi viongozi tugharamie sehemu kubwa ya utunzaji wa vijana hao. Wanapofika wakati wa kuhitaji kuowa, tumekuwa tunawaozesha vijana hao kwa kushirikiana na/au kushauriana na wazazi wao na wenyeji wao. Katika miaka kadhaa ambayo tumekuwa tukiendesha shughuli hizi, tumeweza kupiga hatua kubwa sana kwa msaada wa Mola Mkarimu. Hatukubahatika kupata wafadhili

wowote. Bali tumekuwa tunatumia kidogo tunachopata na tunamshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.) kwa kutubariki. *AL-HAMDULILLAH*!

Tunaendelea kupata maombi ya kujenga Misikiti na vyuo, na ya kupeleka Walimu kutoka sehemu mbali mbali nchini. Lengo letu ni kuimarisha na kupanua aina ya huduma tunazotoa pamoja na kukuza viwango vyake. Katika jumla ya mipango yetu ya baadaye, Mwenyezi Mungu (S.W.) akituwezesha, ni kujenga shule za Kiislamu katika mikoa mbali mbali zikiwa pamoja na Misikiti, Nyumba za kuishi Walimu, Nyumba za kulala Wanafunzi (mabweni) na Zahanati kwa kuwahudumia watu wa maeneo hayo. Mwenyzi Mungu (S.W.) Atuwezeshe, AMIN.

## C. HALI YA JUMUIYA NA MATATIZO YAKE

Jumuiya yetu bado ni changa, tangu tuandikishwe mwaka 1990, shughuli tulizokuwa nazo za kujenga Misikiti, vyuo, na kuviendesha pamoja na kuviimarisha, ni nyingi mno. Hata hivyo, hatuna budi kukiri kwamba uwezo wetu wa kuimarisha shughuli tulizokwishaanza Ki-fedha (mbali na upanuzi tunaokusudia kuufanya) ni mdogo sana. Kwa sababu hii, ili tuweze kunusuru Dini ya Mwenyezi Mungu (S.W.) hatuna budi tutoe mwito kwa Waislamu wenzetu popote

walipo watuunge mkono. Amesema Allah Mkarimu:

***"PINDI MKIINUSURU DINI YA ALLAH, NAYE ATAKUNUSURUNI NA KUZITHIBITISHA NYAYO ZENU"* (Surat Muhammad:Aya7)**

Kwa hakika kila mtenda mema huwa anaitendea nafsi yake. Anayefanya wema kwa kutoa chochote katika mali huwa anaweka akiba kwa Mwenyezi Mungu (SW). Haya yamethibitishwa na Mwenyezi Mungu (SW) katika Qur'ani kwa kusema:

***"NA KHERI YOYOTE MNAYOITANGULIZA KWA AJILI YA NAFSI ZENU MTAIKUTA KWA MWENYEZI MUNGU IMEKUWA BORA ZAIDI NA INA MALIPO MAKUBWA ZAIDI". (Surat Al-Mzzammil:aya 20)***

Licha ya upanuzi wa shughuli zetu, hivi sasa tunayo matatizo mengi ya upungufu wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kuimarisha Majengo tuliyonayo angalau yafikie katika hali ya kuridhisha. Vifaa hivyo ni kama Sementi, Matofali, Nondo, Kokoto, Mabati, Mbao, Mchanga, Vipoza hewa na vinginevyo vingi vinavyoambatana na shughuli za ujenzi. Hali kadhalika, tunao upungufu wa vifaa vya kusomea na kukalia kama Misahafu, Juzuu, Vitabu vya Hadithi na Vitabu vinginevyo, Madawati, Majamvi, Madaftari na Kalamu za kuandikia. Vile vile vinahitajika vifaa vya ofisini kama Meza, Viti, Mashine za kupigia chapa

(Computers/Printers/Scanners etc.) za Kiarabu na Kiingereza, Mitambo ya kuchapishia vitabu (Offset Press), Mashine za kurudufisha (Stencil Machines), Mashine za kutoa nakala (Photocopying Machines).

## D. UENDESHAJI

Kwa kawaida Maimamu katika Misikiti yetu hawalipwi kwa kazi hiyo kutokana na hali yetu nyepesi. Lakini walimu pamoja na wanafunzi tulionao katika maeneo ya vyuo vyetu mbali mbali wanatoka sehemu za mbali na wote wanaishi katika maeneo ya Utendaji wa kazi zao na wanakuwa kwenye mazingira ya Mahitaji yao mbali mbali kama vile Chakula, Nguo na matibabu, huku tukiwa kwa upande wetu tunakabiliana nayo kwa shida kubwa. Walimu hao, ambao wanastahili kupewa angalau posho, wanaendesha kazi zao katika hali ngumu.

Kutokana na matatizo haya, tunatoa mwito kwa ndugu zetu wote kushirikiana nasi, katika kheri hizi kwa kuchangia kadiri ya uwezo wao. Sio lazima watoe fedha taslimu; wanaweza kutoa vifaa au ushauri ili kufanikisha shughuli hizi.

Mwenyezi Mungu (SW) Ametoa mwito kwa kila Muislamu kutenga fungu la kutosha katika mali yake kwa ajili ya kutumikia na kuendeleza

Dini yake. Hivyo, inataka tuwe wepesi katika mambo haya bila ya kuchelea kupungukiwa na mali zetu. Kwa hakika Bwana Mtume (S.A.W.) amesema kutokana na Seyyidina Abu Huraira (R.A.):

***"MALI YA MTU HAIPUNGUI KUTOKANA NA YEYE KUTOA SADAKA"*** **- Muslim**

Kinyume cha kupungukiwa; Mwenyezi Mungu (S.W) Humuongezea mja wake huyo neema za kilimwengu mbalimbali; pamoja na neema za akhera anazomuandalia. Amesema Mola Mkarimu katika Qurani:

***"MKIMKOPESHA ALLAH MKOPO MZURI (KUTOKANA NA MALI ZENU, NGUVU ZENU, WAKATI WENU N.K.) BASI ATAKUZIDISHIYENI NA ATAKUFUTIENI MADHAMBI YENU, NA ALLAH NI MWINGI WA KUSHUKURU. (WAFANYAYO WAJA WAKE KWA AJILI YAKE) NA NI MPOLE MNO JUU YA HAO".*** **(Surat Al- Taghaabuni: Aya 17).**

Katika jumla ya neema ambazo sadaka za mtu zitampatia huko akhera (kutokana na Hadithi ya Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) iliyonakiliwa na Imamu Ahmad(R.A)na pia Ibn Khuzayma (R.A)ni kwamba, sadaka za Muislamu ndizo zitakazokuwa kivuli chake siku ya Kiyama.

Katika Hadithi nyingine iliyopo-kelewa na Sayyidina Muadhi bin Jabal (R.A.) na kunakiliwa na Attirmidhy, Bwana Mtume (S.A.W.) amesema:

***"SADAKA HUFUTA MADHAMBI YA MTU KAMA MAJI YANAVYOZIMA MOTO".***

Na Mwenyezi Mungu (S.W.) Amesema:

***"HAMTAPATA UTUKUFU MPAKA MTOE KATIKA MNAVYOVIPENDA". (Surat Aal Imran: Aya 92).***

Na aghalabu yetu wanadamu, katika tunavyovipenda sana ni pamoja na mali zetu. Mradi tu mtu atoe kwa ajili ya MOLA wake.

Tunachukua fursa hii kuwahakiki-shia Waislamu kwamba chochote wataka-chochangia katika fikra, mawazo, na nguvu basi tutayathamini sana. Na kadri watakachochangia katika mali, ikiwa fedha, nyumba, kiwanja n.k. basi InshaAllah, haitatumiwa mali hiyo ila kwa kuendeleza Dini yetu kwa ajili ya Mola wetu.

Tumenakili anuani na akaunti zetu za Benki katika Katiba hii ili kuwarahisishia ndugu zetu watakaotaka kuchangia kwa kupitia Benki. Na wale wote watakaopenda kutoa michango yao kwa kutoa vifaa au ushauri, basi na waonane na viongozi wa Jumuiya Ofisini, Vituoni au Mazawiyani.

Tunatanguliza shukurani zetu za dhati kwa wote watakaoshirikiana nasi katika kheri hizi kifedha au kwa namna yoyote ile. Na tunawaombea Mwenyezi Mungu(S.W) kwa namna yoyote ile. Na tunawaombea Mwenyezi Mungu (S.W.) Awazidishie kila la kheri Duniani na Akhera - AMIN.

## E. UFAFANUZI WA KIDINI

### (1) KIINI CHA DINI YA KIISLAMU:

Katiba hii ni ya Jumuiya ya KIDINI iitwayo ***"Jumuiya Zawiyatul Qadiriya Tanzania"*** kama jina lenyewe linavyoonyesha, Jumuiya hii imetokana na misingi ya Twariqatul Qadiriya. Na Twariqatul Qadiriya, kama zilivyo Twariqa zote, misingi yake ni Qur'ani na Sunna za Bwana Mtume (S.A.W.); madhumuni yake ni kuendeleza mafundisho ya ki-Twariqa nchini Tanzania.

Kwa kuwa Twariqa ni jambo lisiloeleweka kwa walio wengi, pana umuhimu mkubwa sana wa kuelezea, na pengine kufafanua japo kwa kifupi, misingi na maana ya baadhi ya maneno muhimu yanayohusiana na Twariqa.

Kabla ya kuingia ndani ya chimbuko na chanzo cha Twariqa na Kazi zake, ni muhimu kabisa kwa kila mmoja wetu aelewe kuwa, Dini ya Kiislamu imegawanyika katika sehemu kubwa mbili; nazo ni SHARIA na TWARIQA. Kutokana na kwamba mambo mawili haya ndiyo hasa ***Kiini cha Dini ya Kiislamu***, ndiyo sababu hasa ya Mwenyezi Mungu (S.W) kumleta Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) kwa wanadamu kuja kuwafundisha Ibada hizo.

Neno "Sharia" na "Twariqa" yote yana maana moja - NJIA. Lakini KI-DINI elimu ya

Sharia (au Fiqhi) ni elimu ya ***Ibada za kiwiliwili,*** na elimu ya Twariqa (au Tasawwuf) ni elimu ya ***Ibada za Kiroho.*** Aina zote hizi mbili za Ibada zimetokana na Mwenyezi Mungu (S.W.) na Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) amewafundisha Maswahaba zake (R.A) hata zikatufikia sisi kupitia kwa Maimamu na Masheikh mbali mbali.

## (2) SHARIA NA KAZI ZAKE (3)

Sehemu ya kwanza ni SHARIA yaani FIK-HI. Maana ya Sharia ki-lugha (Kiarabu) ni njia. Na kwa maana ya KI-DINI, Sharia yaani FIK-HI ni Elimu yenye kukusanya hukumu za Kiislamu. Yaani mwenendo ambao kila Muislamu anatakiwa aufuate ki-maisha na ki-ibada kwa manufaa yake Duniani na Akhera.

Kazi ya Sharia ni kushughulikia Ibada zote za kiwiliwili, kama *SWALA, ZAKA, FUNGA, HIJA, NDOA*, kununua, kuuza na mipango/taratibu za Ibada mbali mbali ambazo zimetokana na Qur'ani na Hadithi za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W). Pia, ni elimu ya Sharia, yaani FIK-HI ndiyo ambayo inamtahadharisha mtu na yaliyoha-ramishwa ili ajiepushe nayo. Kwa mfano: kuua, zinaa, kuiba, kulewa pombe na vileweshaji vingine, kutukana, kusema uongo, kugombanisha watu, kudhulumu

na maharamisho mengine. Kama alivyosema Bwana Mtume (S.A.W):

***"HAKIKA HALALI IKO WAZI NA HAKIKA HARAMU IKO WAZI, NA KATI YA HALALI NA HARAMU KUNA MAMBO YENYE KUTATANISHA AMBAYO HAWAYAJUI WENGI MIONGONI MWA WATU BASI (MTU) MWENYE KUEPUKA MAMBO YATATANISHAYO, HAKIKA ANAKUWA KAJITAKASA KIKWELI KWA DINI YAKE NA (HESHIMA YA) CHEO CHAKE. NA MWENYE KUJIINGIZA KATIKA MAMBO YATATANISHAYO (ATAKUWA) AMEINGIA KATIKA HARAMU. NI KAMA (KWAMBA) MCHUNGA ANAYECHUNGA (WANYAMA WAKE) PEMBEZONI MWA MIPAKA (YA SHAMBA LENYE MIMEA). HUHOFIWA (BILA SHAKA YOYOTE KUWA, WANYAMA WAKE HAWA AWACHUNGAO WATAINGIA SHAMBANI NA KULA HUMO). JUENI VYEMA YA KWAMBA HAKIKA KILA MFALME ANAYO MIPAKA YAKE. JUENI VYEMA PIA KUWA, KWA HAKIKA MIPAKA YA MWENYEZI MUNGU NI MAHARAMISHO (MAKATAZO) YAKE. JUENI, ELEWENI VYEMA PIA KUWA, KWA HAKIKA KATIKA MWILI (WA MWANADAMU) KUNA PANDE LA NYAMA (AMBALO) LINAPOTENGENEA (PANDE HILO LIKATAKASIKA) HUTENGENEA MWILI WOTE (UKATAKASIKA), ELEWENI (FAHAMUNI) KUWA (PANDE HILO) NI MOYO".*** Bukhari na Muslim kutoka kwa Swahaba Nuuman bin Bashir (R.A.)

Katika Elimu ya Shariya mtu anaweza kuzama sana katika Ibada hiyo (ya kiwiliwili) na atapata kufahamika kuwa ni Mwana-chuoni wa kusifiwa ulimwenguni. Lakini ifahamike wazi kuwa ukamilifu wa Ibada za Kiislamu haujapatikana kwani Ibada za kiroho zitakuwa zimekosekana. Hapo ndipo wenye busara wanapolazimika

kutafuta elimu ya kiroho kwa wenye kuwa nayo.

Mfano mzuri ni Imamu Abuu Hamid Muhammad ibn Muhammad Al-Ghazali (R.A.)

Imamu Ghazali (R.A.) anatambuliwa Duniani kote kuwa ni Mwana-chuoni na Mcha-Mungu mkubwa sana. Katika kitabu chake ***Al-Mun-qidh Min al-Dhalalah*** (yaani "uokofu kutokana na upotovu"), Imamu Ghazali (R.A.) anaandika:

***"BAADA YA KUZITAMBUA VYEMA ELIMU HIZI (ZA SHARIA), NILIANZA KUTAFITI NYENDO NA TARATIBU ZA MASUFI, NILIKUJA KUTAMBUA KWAMBA NJIA (TWARIQA) ZAO ZINAMPELEKEA MTU KWENYE UHAKIKA WA KINADHARIA NA KIVITENDO. KIINI CHA ELIMU YAO NI KUITENGENEZA NAFSI NA KUIPA NGUVU DHIDI YA MATAMANIO NA MAASI ILI MOYO UEPUKANE NA MAWAZO YA YEYOTE ASIYEKUWA MWENYE-ENZI MUNGU (S.W) NA UNAWIRIKE NA UTAJO WAKE".***

Ndugu Waislamu, hii inaonyesha namna elimu ya Sharia inavyoweza kumpa mtu utukufu mbele ya watu na akakosa ukaribifu kwa Mwenyezi Mungu (S.W.) kwa kukosa elimu ya Twariqa (Ibada ya kiroho).

Kwa hivyo basi, sisi tufanyao Ibada hizi za Kiroho (Twariqa) ikiwa ni katika kukamilisha Uislamu (baada ya Ibada za kiwiliwili) tumeona ni heri tuwe na UMOJA, umoja ambao ndiyo msingi uliotumika katika kuanzisha **JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA.**

## (4) TWARIQA NA KAZI ZAKE:

Sehemu ya pili ya Dini ni Twariqa (yaani TASAWWUF).

Maana ya Twariqa Ki-lugha ni NJIA kama ilivyokwishatangulia kuelezwa, na kwa maana ya KI-DINI: ***"Twariqa ni mwenendo wa Ibada ulio bora, mwepesi na wa haraka kumfika Mwenyezi Mungu (S.W.)".***

Kazi yake ni kushughulikia Ibada zote za Ki-roho yaani; kumfundisha mtu Uislamu na kumlea ili ampende sana Mwenyezi Mungu (S.W.) na Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) kwa kuwataja sana kwa ulimi wake na Moyoni mwake. Pia, kumfanya Muislamu huyo awe mnyenyekevu sana, mwenye adabu sana na mtekelezaji mzuri sana wa amri zote za Dini. Yaliyoamrishwa ayatekeleze vizuri na yaliyokatazwa ajitenge nayo.

Kadhalika, Twariqa ambayo imejengwa juu ya nguzo ya Tawhid, ndiyo inayomfundisha Muislamu namna ya kuusafisha moyo wake na maasi ya ndani na kuujaza Moyo na mema kama ifuatavyo:

i. ***Kumuondoshea kiburi na kumfanya awe mwenye adabu;***
ii. ***Kumuondoshea hasadi na kumfanya awapende na kuwapendelea mema wenzake;***
iii. ***Kumuondoshea tabia ya kujiona na kumfanya awe mnyenyekevu;***

iv. ***Kumuondoshea tabia ya kujionyesha kwa watu na kumjengea tawhid;***
v. ***Kumuondoshea tabia ya kuwawekea wenzake undani na kumtia usafi wa Moyo;***
vi. ***Kumuondoshea ghadhabu na kumfanya awe mwenye subira na mtu wa nasaha;***
vii. ***Kumuondoshea chuki na kujaza mapenzi kwa Muumba na viumbe;***
viii. ***Kumuondoshea dharau na kumfanya awe mwenye kuheshimu wenzake;***
ix. ***Kumuondoshea matamanio ya nafsi na kumfanya awe mtu mwenye kutosheka na neema alizopewa na Mwenyezi Mungu (S.W.)***

Maasi yote ya Nje na ya Ndani ni maadui wa Nafsi zetu. Lakini hapana shaka maasi ya ndani ni mabaya zaidi na ni vigumu zaidi kuyashinda na kujitakasa nayo. Na pindi itokeapo mtu akajitahidi sana kujitakasa basi Mwenyezi Mungu (S.W.) humpenda sana mtu huyo. Mungu Amemsifu mtu huyo kwa kusema:-

***"HAKIKA AMEFAULU ALIYEJITAKASA". (Suratul Aalaa: Aya 14).***

Kwa jumla, kazi ya kujitakasa na maasi ya nje na ndani ni ya lazima mno kwa kila mtu ili apate uongofu na mafanikio Duniani na Akhera. Mwenyezi Mungu (S.W.) Amesema:

***"NA ACHENI DHAMBI ZILIZO DHAHIRI NA ZILIZOFICHIKA". (Surat Al-Anam: Aya 120).***

Kadhalika Mwenyezi Mungu (S.W.) Amesema:

***"SEMA,(EWE MUHAMMAD) HAKIKA MOLA WANGU AMEHARAMISHA MACHAFU YA NJE NA YA NDANI"*. (Suratul Aaraf: Aya 33)**

Mtu aliye mzingatifu hana budi kushughulika sana na kujiuliza vipi atajiepusha na hayo madhambi au machafu ya ndani? Kwa kuongezea, vipi Mwislamu atausafisha Moyo wake na kuupa nguvu dhidi ya matamanio mabaya ya Nafsi yake na dhidi ya Shetani?

Kwa kutokuelewa, mtu anaweza kudhani kwamba kazi hii ni rahisi na haihitaji msaada wowote. Uzito na ugumu wa kazi hii tunaweza tu kuufahamu tukizingatia maneno ya Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.). Baada ya kuiteka Makka na kupata ushindi mkubwa sana katika vita vya HUNAYN, Waislamu walijisikia kumaliza **Vita vya kuikomboa Dini yao** dhidi ya Makafiri wa Bara Arabu. Wakati huo Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) alikuwa amebakisha chini ya miaka miwili ya kuishi (lakini bila shaka wao hawakuelewa hayo). Walipokuwa wanarudi Madina Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) na Maswahaba zake(R.A), njiani Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) aliwaambia:

***'Tunarudi sasa kutoka katika vita vya Jihadi ndogo, tunakwenda katika vita vya Jihadi***

***kubwa'. Mmoja katika Maswahaba akamuuliza: 'Ipi hiyo Jihadi kubwa, ewe Mjumbe wa Mwenye-Enzi Mungu?' Na Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) akajibu: 'Ni vita vya kupigana na nafsi'.***

Mwenyezi Mungu (S.W.) Amethibitisha katika Qur'ani uzito wa Jihadi hii kwa kusema:

***"HAKIKA NAFSI INAAMRISHA MAOVU"* (Suratu Yusuf: Aya 53).**

Hii ni ithibati kwamba ni kweli kabisa, Wanadamu tunapigwa vita sana na Nafsi zetu. Na tusipoangalia, zitatuangamiza. Hivyo, hatuna budi kutafuta silaha ya kupigania vita hivi. Kama ilivyo kawaida, jawabu ya maswali yetu yote Waislamu tunatakiwa turudi katika Qur'ani na Sunna za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.). Kwa ufupi, ufumbuzi wa matatizo haya unapatikana katika malezi na Ibada za KI-TWARIQA.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (S.W.) Atuwezeshe na Atusaidie kuzitakasa Nafsi zetu, ili tuwe miongoni mwa waja waliofaulu. Amin.

## (5) MSINGI WA TWARIQA:

Mwenyezi Mungu (S.W.) Ameiteremsha Twariqa kwa Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) kupitia kwa Seyyidina Jibril (A.S.), na kutoka kwa

Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) ikatiririka mkono kwa mkono mpaka ikatufikia sisi.

Twariqa na Sharia ni misingi ya DINI ya Kiislamu na ni vitu vilivyolazimiana. Mwenyezi Mungu (S.W.) Amesema katika Kitabu Chake:

***"HAKIKA MWENYEZI MUNGU (S.W.) AMEWAFANYIA IHISANI KUBWA WAUMINI/ WAISLAMU ALIPOWALETEA MTUME MIONGONI MWAO, ILI AWASOMEE AYA ZAKE (AWAFUNDISHE DINI YAKE), NA AWATAKASE (YAANI AWAFUNDISHE TWARIQA/TASAWWUF NA AWAFUNDISHE QUR'ANI (YAANI SHARIA/FIK-HI ILI WAJUE YALIYOHALALISHWA NA YALIYOHARAMISHWA), NA HEKIMA NA IJAPOKUWA KABLA (YA KUPELEKEWA MTUME) WALIKUWA KATIKA UPOTEVU ULIO WAZI".*** **(Suratul Aal Imran-Aya 164**)

Kwa kifupi maana ya Aya hii, Mwenyezi Mungu (S.W.) Anatuarifu kwamba ameileta DINI Yake na Mtume Wake (S.A.W.) kwa ajili ya:

(a) Kuwatakasa Waislamu - yaani kuwafundisha Twariqa/Tasawwuf;

(b) Kuwafundisha Kitabu - yaani kuwafundisha Sharia/Fik-hi, ili wajue mambo yaliyohalalishwa na yaliyoharamishwa pamoja na Ibada zao.

(c) Kuwafundisha Hekima yaani Hakika na Maarifa.

Hali kadhalika, Aya hii inaonyesha kazi alizoletewa Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) kwa wanadamu. Vile vile, Aya hiyo inatuonyesha umuhimu wa Twariqa katika DINI ya Kiislamu.

Lakini, kwa bahati mbaya watu wengi hushughulikia Sharia tu na wakasahau kabisa TWARIQA. Kwa hali hii si rahisi kupata mafanikio. Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) amesema:

***"SHARIA NI KAMA JAHAZI NA TWARIQA NI KAMA BAHARI NA HAKIKA NI KAMA CHAZA NA MAARIFA (KUMJUA ALLAH) NI KAMA LULU (AMBAYO HUPATIKANA BAHARINI). BASI MTU AITAKAYE LULU NI LAZIMA APANDE JAHAZI, KISHA APITE (KWA JAHAZI HILO) KATIKA BAHARI, NDIPO ATAKAPOIFIKIA LULU. NA YULE AMBAYE ASIYEFUATA UTARATIBU HUU HAWEZI KUFIKA KWENYE LULU."*** **(Hadithi-Kitabu:Tadhkiratul Waidhina).**

Maana ya Hadithi hii, inatuonyesha hasa ulazimiano uliopo kati ya TWARIQA na SHARIA. LULU hapa mfano wake ni PEPO, na LULU haipatikani popote isipokuwa baharini tu. Hivyo, Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) anatuambia kuwa ikiwa tunataka LULU (yaani PEPO), ni lazima tupande ndani ya Jahazi (SHARIA) kisha tuingie ndani ya Bahari (TWARIQA) ndipo tutapofika kwenye LULU (PEPO). Kwa kifupi, ikiwa tunataka kuingia PEPONI ni lazima tuitumikie SHARIA vizuri na hapo hapo tuitumikie TWARIQA vizuri ndipo tutakapofanikiwa.

## (6) IJAZA:

Ijaza ni namna/njia ya kuipata Twariqa, yaani ni kiingilio katika Twariqa. Ki-Twariqa, neno hili hutumika kujumuisha "TALQIN" na "MUBAYAATU", yaani kuchukua ahadi mbele ya Sheikh ya kufungamana na Ibada ya Mwenyezi Mungu (S.W.).

Asili ya Ijaza ni kama ifuatavyo: Wakati Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) alipokuwa Madina, aliendewa na Sayyidina Ali bin Abi Twalib (K.W.) na kumuomba amfundishe njia ya kumfika Mwenyezi Mungu (S.W.) yenye sifa tatu:

Kwanza: Njia iliyo fupi kuliko zote; Pili:Njia iliyo bora kuliko zote; na Tatu: Njia iliyo nyepesi kuliko zote.

Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) aliemewa na alikaa kimya kusubiri WAHYI. Baada ya muda mchache, Seyyidina Jibril (A.S.) alimtokea Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) na kumpa jibu la swali la Seyyidina Ali (K.W). Jibu hilo ni **LAA ILAHA ILLA LLAHU.** Hii ndiyo iliyokuwa sababu ya kuteremshwa Aya ifuatayo:

***"JUA YA KWAMBA HAKUNA AABUDIWAYE KWA HAKI ILA MWENYE-ENZI MUNGU, NA OMBA MSAMAHA KWA DHAMBI ZAKO NA ZA WAISLAMU WANAUME NA WANAWAKE....".*** **(SURATU MUHAMMAD AYA 19)**

Aya hii ndiyo iliyokuwa na utaratibu wa kuipata Twariqa - yaani ***Mubayaatu*** au ***Talqinul***

**IJAZA.** Baada ya kushuka Aya hii, Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) alipewa IJAZA na Sayyidina Jibril (A.S) naye akaanza kumpa IJAZA Seyyidina Ali (K.W) na aliwapa Ijaza Maswahaba zake wote wanaume na wanawake (R.A). Hili halikuwa jambo la hiari kwani ilikuwa amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu (S.W). Hivyo Maswahaba wote (R.A)wakawa ni Muridi wa Bwana Mtume Muhammad (S.A.W).

Itakumbukwa kwamba wakati mtu anapoingia katika Uislamu lazima atamke kwa Ulimi Shahada mbili na akiri kwa moyo:

"***ASH-HADU AN LAILAHA ILLA LLAHU WA ASH-HADU ANNA MUHAMMADA RASULULLAHI***"

Hivyo hivyo Muislamu anapoingia katika Twariqa hutamkishwa tamko la "LAILAHA ILLA LLAHU" mara tatu. Baada ya kutamkishwa lAILAHA ILLA LLAHU mara tatu ndipo tena anakuwa Muridi wa Twariqa iliyokusudiwa iwe QADIRIYA au Twariqa nyingine.

Mwenyezi Mungu (S.W.) Amesema:

"***HAKIKA WALE WANAOFUNGAMANA NA WEWE WAMEFUNGAMANA NA MWENYEZI MUNGU, MKONO WA MWENYEZI MUNGU UKO JUU YA MIKONO YAO. BASI AVUNJAE AHADI HIZI ANAIDHURU NAFSI YAKE, NA ANAYETEKELEZA ALIYOMUAHIDI MWENYE-ENZI MUNGU BASI MWENYEZI MUNGU ATAMLIPA UJIRA MKUBWA".*** **(Suratul Fat-h: Aya 10).**

Aya hii inatufundisha umuhimu wa kuchukua ahadi ya Twariqa. Jambo hili limeendelea tangu zama za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.). Bidii ya kueneza Twariqa kwa Waislamu ilifanyika na kuendelea mkono kwa mkono hadi leo. Twariqa ni jambo la lazima kwa Waislamu wote na wala siyo Sunna wala jambo la hiari kama baadhi ya walio wengi wanavyofikiri.

## (7) MALEZI YA TWARIQA:

Miongoni mwa kazi kubwa za Twariqa ni kushughulikia Ibada za ndani ya mwili wa Binadamu, hasa kuusafisha Moyo na kwa ujumla kuzikamilisha Ibada zote za nje na ndani.

Twariqa ndiyo hasa inayomlea mtu mpaka akawa mwenye adabu sana, mtekelezaji mzuri wa amri za Mwenyezi Mungu (S.W.), na msikivu na mtiifu mpaka akawa safi Kiroho na kuwa mpenzi wa Mwenyezi Mungu (S.W.) na pia akawa mpenzi wa Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.).

Hapana shaka yoyote, Uislamu unahitaji Imani, yaani ***kuamini.*** Bila ya Imani hapana Uislamu. Imani pahala pake ni Moyoni, na Ucha-Mungu, unaotokana na Ibada, pia uko ndani ya Moyo.

Hivyo utaona Moyo ndiyo shina la Uislamu, na ndiyo shina la Ibada, unyenyekevu, hofu, kupenda na ndilo shina la Ucha-Mungu. Na bila

ya Moyo kuwa safi hapana Ibada wala mafanikio yoyote isipokuwa hasara tupu. Tambua na ujue kwamba kazi ya kusafisha Moyo ni kazi ya Twariqa. Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) amesema:

***"...HAKIKA KATIKA MWILI (WA MWANADAMU) KUNA PANDE LA NYAMA, LINAPOTENGENEA (LIKATAKASIKA) HUTENGENEA MWILI WOTE. ELEWENI KUWA (PANDE HILO) NI MOYO".*** **(Bukhari na Muslim).**

Kwa kuwa Moyo ndiyo shina, yaani asili ya kila kitu, basi Shetani huwa anauandama kila wakati ili auharibu kama Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) alivyosema:

"***SHETANI HUUMEZA MOYO WA MWANADAMU. WAKATI (MWANADAMU) ANAPOMTAJA MWENYEZI MUNGU, SHETANI HUJITENGA NAYE. NA ANAPOSAHAU KUMTAJA MWENYEZI MUNGU, SHETANI HUUMEZA TENA MOYO WAKE".*** **(Ahmad).**

Kazi kubwa ya Twariqa ni kumlea Mtu. Inatakiwa mtu ampende sana Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kumdhikiri sana. Kwa kufanya hivyo ndivyo anaitakasa nafsi yake na moyo wake na ndiyo anaepukana na Shetani. Kutokana na Sayyidina Abdillahi ibn Amr (R.A.), Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) alikuwa akisema:

***"KILA KITU KINA KISAFISHO CHAKE, NA KISAFISHO CHA NYOYO NI DHIKRI YA MWENYEZI MUNGU(YAANI UTAJO). NA HAPANA KITU CHOCHOTE KINACHOWEZA KUMUOKOA MTU KUTOKANA NA ADHABU ZA MWENYEZI***

***MUNGU KULIKO DHIKRI YA MWENYEZI MUNGU"*. (Ibn Abi Duniya).**

Kwa ufupi, umuhimu wa Twariqa unaweza kuonekana kwa kuzingatia Aya ifuatayo:

***"HAKIKA WAUMINI WA KWELI NI WALE AMBAO ANAPOTAJWA MWENYEZI MUNGU, NYOYO ZAO HUJAA KHOFU (YAANI HUTAHARUKI);NA WANAPOSOMEWA AYA ZAKE HUWAZIDISHIA IMANI, NA WANAMTEGEMEA MOLA WAO PEKE YAKE"*. (Suratul-Anfal: Aya 2).**

Sehemu kubwa kuliko zote ya malezi ya Twariqa ni katika Kumdhikiri Mwenyezi Mungu (S.W.). Neno DHIKRI lina maana ya Kumkumbuka, Kumtaja, Kumpwekesha, Kumtukuza, Kumtakasa na Kumsifu Mwenyezi Mungu (S.W.). Kusoma Qur'ani na Kusali pia ni katika Kumdhikiri Mwenye-Enzi Mungu (S.W.). Ni amri yake Mwenyezi Mungu (S.W.) kwamba kila Mwislamu amdhikiri Mola wake nyakati zote. Hii ni kwa faida yetu wenyewe Waislamu kwani hakuna Ibada bora zaidi kuliko Dhikri. Sayyidina Abii Said Al-Khudhry (R.A) ameripoti kwamba Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) aliulizwa:

***"...NANI KATIKA WAJA ATAKUWA NA DARAJA KUBWA KULIKO WOTE MBELE YA MWENYEZI MUNGU SIKU YA KIYAMA?" BWANA MTUME (S.A.W.) AKAJIBU: "WENYE KUMDHIKIRI MWENYEZI MUNGU SANA" HAPO AKASEMA SAYYIDINA ABII SAID AL-KHUDHRY (R.A.): "EWE MJUMBE WA MWENYEZI MUNGU, SASA VIPI WENYE KUPIGANA VITA KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU!" BWANA MTUME (S.A.W.) AKAJIBU: "LAITI ANGELIPIGANA MTU NA MAKAFIRI NA WENYE KUMSHIRIKISHA MWENYEZI MUNGU***

***MPAKA UPANGA WAKE UKAKATIKA, BASI BADO WENYE KUMDHIKIRI MWENYEZI MUNGU NI BORA ZAIDI WA DARAJA MBELE YA MOLA".*** **(Attirmidhy).**

Kwa upande mwingine, Qur'ani imetaja Dhikri kuwa ndiyo silaha kubwa ya kumsaidia mtu kupigana na nafsi yake (tazama Qur'ani: 8:45). Ndiyo itakayompa utulivu wa moyo wake (tazama Qur'ani: 13:28). Ndiyo itakayompatia msamaha na ujira mkubwa kutoka kwa Mola wake (tazama Qur'ani: 33:35) na, kwa jumla, ndiyo itakayomuwezesha mtu kufaulu (tazama Qur'ani: 8:45, 62:10).

## (7) ZAWIYA:

Zawiya ni mahala/sehemu iliyo maalumu KI-DINI kwa ajili ya malezi ya Mtu au kikundi cha Watu katika Kumtaja/Kumkumbuka/Kumfikiri sana Mwenyezi Mungu (S.W) kwa namna moja au nyingine. Zawiya la kwanza katika Uislamu ni ile sehemu ya Pango la **Jabal Hira (Makka**) alipokuwa Bw Mtume (S.A.W) akimdhikiri sana Mwenyezi Mungu (S.W), **ALLAH ALLAH ALLAH** kabla Bw mtume (S.A.W) kupewa Utume. Ulipofika wakati mnasaba alipewa Utume na kushushiwa Quran Aya tano za mwanzo hapo hapo pangoni. Suratul Alaq (96):1-5.

Zawiya la pili katika Uislamu ni ile sehemu katika nyumba ya Arqama aliposilimia Sayyidina

Umar bin Khatwabi (R.A). Nyumba ya Arqama (R.A) waislamu walikuwa wakikusanyika kwa ajili ya kumtaja Mwenyezi Mungu (S.W) na kuswali. Nyumba hii haikuwa Msikiti bali ni Zawiya. Kumbukeni kwamba Msikiti wa kwanza katika Uislamu ulijengwa Madina (Masjid Qubaa) baada ya Hijra ya Bw.Mtume Muhammad (S.A.W).

Zawiya la tatu katika Uislam, Wakati Bwana Mtume (SAW) alipohamia Madina lilipatikana Zawiya kubwa la Aswhabu Suffa (R.A) mahala walipokutana Maswahaba zaidi ya Mia nne (400) Mwenyezi Mungu (S.W) alisisitiza Bwana Mtume (SAW) awe karibu nao sana.

***"ISUBIRISHE NAFSI YAKO KWA KUJIWEKA NA WANAOMUABUDU (WANAOMLINGANIA) MOLA WAO ASUBUHI NA JIONI, HALI YA KUWA WANATAKA RADHI ZAKE. wALA MACHO YAKO YASIWARUKE KWA KUFUATA MAMBO YA DUNIA. WALA USIMFUATE YULE AMBAYE TUMEMSAHAULISHA MOYO WAKE NA DHIKRI YETU NA AKAWA ANAFUATA MATAMANIO YAKE NA YAKAWA MAMBO YAKE YAMEPITA MIPAKA.*** **(Suratul Kahf: 28)"**

Pia Mwenyezi Mungu akaelezea tena hali ya Aswahabu Suffa (R.A) katika Suratul Baqara aya 273.

"***(Wapewe hizo Sadaka) Mafakiri waliozuiwa katika Njia za mwenyezi mungu, wasioweza kwenda huko na huko katika Ardhi (kufanya kazi ya kutafuta Riziki), asiyewajua hali zao***

***anawadhania kuwa ni Matajiri kwa sababu ya kujizuiya kwao na kuomba. Utawafahamu (kuwa Wahitaji) kwa alama zao zinazoonesha Ufakiri, Lakini hawawaombi watu wakafanya Ung'ang'anizi. Na mali yoyote mnayoitoa, basi kwa Yakini Mwenyezi Mungu anaijua (atakulipeni)"***

Katika wakati wa Ukhalifa wa Sayyidina Umar bin Khatwabi (R.A.), unapatikana ushahidi mwingine wa Zawiya. Nchi ya Misri (Egypt) ilitekwa na jeshi la Kiislamu lililokuwa likiongozwa na Seyyidina Amr bin Al-Aas (R.A.) Baada ya hapo, Sayyidina Umar (R.A.) alimteua Sayyidina Amr (R.A.) kuwa Gavana wake huko Misri. Sayyidina Amr (R.A.) alijenga Msikiti wa kwanza huko unaoitwa **MASJID AMR IBN AL-AAS**. Kama kawaida, Mafunzo ya Dini yalikuwa yakitolewa hapo Msikitini. Baadaye ulijengwa Msikiti wa pili na ukoo wa mama Fatuma Al-Zahrai (R.A.) ulioitwa **AL-AZHAR**. Pahala palipokuwa pakitolewa mafunzo ya Dini katika **AL-AZHAR** palikuwa pakiitwa **HALAQAH**; na pale palipokuwa pakitolewa mafunzo hayo katika **MASJID AMR BIN AL-AAS** palikuwa pakiitwa "**ZAWIYA**".

Tofauti ya mwahala muwili humo ni kwamba wasomeshaji wa **HALAQAH** walikuwa wakilipwa mshahara kutoka Serkalini, na wale

wa **ZAWIYA** walikuwa wakijitolea. Neno Zawiya linatumika sasa kumaanisha mahala wanapokutana Muridi (wafuasi wa Twariqa) kwa ajili ya mafunzo ya malezi ya Ki-Dini. Na Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) ameletwa kwa kazi hiyo pia. Mwenyezi Mungu (S.W) Amesema:

***"YEYE (MWENYEZI MUNGU (S.W.) NDIYE ALIYEMLETA KWA WATU WASIOJUA KUSOMA, MTUME ANAYETOKANA NA WAO WENYEWE, ILI AWASOMEE AYA ZAKE, NA AWATAKASE (NA MACHAFU) NA AWAFUNZE KITABU (QUR'ANI) NA HEKIMA". (*Suratul-Jumaa: Aya 2).**

Kazi ya kuusafisha Moyo/Nafsi ni muhimu kabisa kwa kila Muislamu awe Muridi au si Muridi, kwani mtu ye yote akishaisafisha NAFSI yake moja kwa moja anapata mafanikio makubwa.

Njia bora na ya uhakika ya kumsaidia mtu kuhifadhi viungo vyake na kumtakasa Moyo wake pamoja na kujifundisha Adabu za KI-DINI hutokana na Malezi ya Ki-Twariqa, yaani kukaa na viongozi wanavyuoni wa Twariqa (R.A). Maswahaba (R.A.) walifanikiwa kwa wepesi na haraka mno katika kujenga Imani zao na Ucha-Mungu wao, kwa kujiweka chini ya malezi ya Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.), na waliofuata, yaani wanafunzi wa Maswahaba walifanikiwa kwa kukaa na Maswahaba (R.A.); na waliokuja baada yao nao walifanikiwa kwa kukaa chini ya ulezi na uongozi wa wanafunzi

wa Maswahaba (R.A.), hali hii imeendelea hadi sasa. Wote wenye kufanikiwa huwa wamepata uongozi na malezi ya Ki-Twariqa. Ni vigumu mno kwa mtu kuongoka kwa njia nyingine. Mwenyezi Mungu (S.W.) Amesema:

***"ISUBIRISHE NAFSI YAKO KWA KUJIWEKA NA WANAOMUABUDU (WANAOMLINGANIA) MOLA WAO ASUBUHI NA JIONI, HALI YA KUWA WANATAKA RADHI ZAKE. wALA MACHO YAKO YASIWARUKE KWA KUFUATA MAMBO YA DUNIA. WALA USIMFUATE YULE AMBAYE TUMEMSAHAULISHA MOYO WAKE NA DHIKRI YETU NA AKAWA ANAFUATA MATAMANIO YAKE NA YAKAWA MAMBO YAKE YAMEPITA MIPAKA".*** *(*Surat Al-Kahf: Aya 28).

Katika Aya hii Mwenyezi Mungu (S.W.) Anatuamrisha tuwe chini ya ulezi wa viongozi wazuri ili tupate kuongoka, na kuwa tufanye subira tunapokuwa katika malezi na wala tusibabaike na maneno na vitendo vya watu waovu na wala tusifuate matamanio ya Nafsi zetu, hapo ndipo tutakapoongoka.

Tunakuomba Mola wetu Mtukufu Utuwafikishe na hayo. AMIN.

## (8) MADHEHEBU ZA TWARIQA:

Kama zilivyo madhehebu za Sharia, ndivyo zilivyo madhehebu za Twariqa. Madhehebu zote hizi za TWARIQA zinatokana na misingi ya Qur'ani na Hadithi za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W), kama zilivyo madhehebu

za Sharia. Shabaha na madhumuni ya madhehebu zote hizi za Twariqa ni kumfanya mtu awe mzuri na amfike Mwenyezi Mungu (S.W) kwa usalama, kama alivyosema Mwenye-Enzi Mungu (S.W):

"***SIKU AMBAYO HAYATAMFAA (MTU) MALI WALA WATOTO ISIPOKUWA (ATASALIMIKA TU MTU) AMBAYE ATAKUJA KWA MWENYEZI MUNGU NA MOYO ULIOSALIMIKA (ULIOTAKASIKA***)".

(Surat Ash-Shuaraa: Aya 88-89).

Ewe Mwenyezi Mungu (S.W.) Tusaidie tuwe katika watu watakaosalimika. AMINA.

Katika ulimwengu zipo Twariqa nyingi sana ambazo zinaongozwa na viongozi mbali mbali. Na kwa uchache kabisa hapa tutazitaja baadhi yake tu ambazo ni kama: Qadiriya, Shadhuliya, Naq-shabandiya, Rifaiya, Dusuqiya na nyingine nyingi.

Hizi Twariqa hujulikana kwa majina ya Masheikh walioziongoza kama yajulikanavyo madhehebu za Sharia, yaani madhehebu ya Imamu Hanafi, Imamu Malik, Imamu Shafii na Imamu Hanbali (R.A.) na mengineyo. Kwa mfano Twariqatul Qadiriya kiongozi wake ni Seyyidina Abdul Qadir Jaylaniy (K.S.), Twariqatul Shadhuliya kiongozi wake ni Seyyidina Abul Hassan Shadhuliy (R.A.) na ni vivyo hivyo ndiyo zilivyo Twariqa nyinginezo.

## (9) TWARIQATUL QADIRIYA:

Hii Twariqatul Qadiriya ni mojawapo ya Twariqa zilizopo katika Dini Duniani kote. Utungo wa mapokezi yake **(SILSILAH)** umeunganika kutoka kwa Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) kuja kwa Seyyidina Ali (K.W.) na kutiririka mpaka kwa Seyyidina Abdul Qadir Jaylaniy (K.S.) na hatua kwa hatua hatimaye ikatufikia sisi. (Kama inavyoonyesha katika Kiambatanisho ‘A’).

Twariqa hii imechukua jina lake kutoka kwa mkubwa wa Mawalii wote, Seyyidina Abdul Qadir Jaylaniy (K.S.). Bwana huyu alizaliwa mwaka 470 baada ya Hijra na kufariki mwaka 561 Hijiriya. Alifanya kazi kubwa sana katika kuhuisha Uislamu na aliheshimiwa sana katika wakati wake na hadi hii leo.

Na Twariqa nyinginezo zote mitiririko ya mapokezi yao imekwenda mkono kwa mkono kutoka kwa Bwana Mtume (S.A.W) mpaka kuwafikia viongozi wao. Kwa hiyo Twariqa siyo jambo geni au lisilokuwa na umuhimu wowote kama watu wengine wanavyofikiria. Viongozi wengi wakubwa waliopita katika DINI ambao wanatajikana mpaka leo hii wamepata Utukufu wao kwa kupitia katika mwenendo huu wa Twariqa.

Kwa kumalizia Jumuiya yetu hii ni sehemu tu ya Twariqatul Qadiriya ambayo inafuata

muongozo wa Sheikh Uweis Bin Muhammad El-Qadiry (R.A). Sheikh Uweis (R.A) alikuja hapa Tanzania kutoka Barawa, Somalia. Silesile yake imeungana na ya Seyyidina Abdul Qadir (K.S.). Sheikh Uweis (R.A.) alichukua Twariqa kutoka kwa Seyyidina Mustafa bin Salman El-Qadiry (R.A.). Baina ya Sheikh Uweis (R.A) na Seyyidina Abdul Qadir (K.S) walipita Masheikh wakubwa wa Twariqa hii 22 (R.A.). Kutoka kwa Sheikh Uweis (R.A.), Twariqa imetufikia sisi kupitia kwa Mlezi wa Roho zetu na muasisi wa Jumuiya yetu hii, Mpenzi wetu Al-Haj Sheikh Muhammad Nassor Abdulla El-Qadiry (R.A.). Tukianza kwa Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) kupitia **Silsilah** hii ya Twariqa yetu, Sheikh Muhammad Nassor Abdulla (R.A) ni Kiongozi wa 36.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu (S.W) Ajaaliye Twariqa zote kwa ujumla ziendelee katika kuwaongoza Waislamu, na sisi kadhalika wanajumuiya na wafuasi wote wa Twariqatul Qadiriya, Mwenyezi Mungu (S.W) Atujaaliye tushikamane tuwe Wanafunzi wazuri mpaka mwisho wa Ulimwengu. **Amin.**

Katika kumaliza utangulizi huu wa Katiba hatuna budi kusisitiza umuhimu wa malezi ya Ki-Twariqa katika Dini. Kwani mafunzo na malezi ya Twariqa yanajumuisha namna zote za Ibada zilizomo ndani ya Qur’ani na zilizofundishwa na

Bwana Mtume Muhammad (S.A.W). Utaratibu wa kutoa mafunzo haya pia umeigwa moja kwa moja kutokana na ule alioutumia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) kwa Maswahaba zake (R.A.). Na hapa ndipo penye siri ya Uislamu. Kufuatana na utaratibu huo, mafunzo ya Ki-Twariqa yanasisitiza kwenye vitendo na mikutano ya mara kwa mara na ya ana kwa ana baina ya Muridi na Sheikh wake. Hivyo ndivyo Bwana Mtume (S.A.W.) alivyosomeshwa na Sayyidina Jibril (A.S.) na ndivyo yeye (S.A.W.) alivyowasomesha Maswahaba wake (R.A.), na waliowafuata Maswahaba nao waliendelea vivyo hivyo hadi leo.

## (10) MWISHO:

Tunapenda kusisitiza kwamba, Jumuiya yetu hii ni ya Ki-dini. Haihusiani na wala haitojihusisha na jambo lolote lililo nje ya Uislamu, au lenye kwenda kinyume na mafundisho yake. Kimsingi, shughuli zetu zote zitaendelea kuelekezwa katika kuuendeleza Uislamu na kuwanufaisha Waislamu. Hata hivyo, hatutowazuia wasio Waislamu kufaidika na huduma zetu.

Hali kadhalika, tutajitahidi kadri iwezekanavyo kushirikiana na pia kusaidiana na Jumuiya zote za Kiislamu katika mambo yanayoafikiana na Qur'ani na Sunna za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.). Katika nyanja

ambazo Jumuiya hii inatofautiana na Jumuiya nyenginezo, juhudi zitapitishwa kuhakikisha kwamba tofauti hizo hazisababishi kutoelewana, seuze kuhasimiana. Ikitokea Jumuiya, au makundi mengineyo, kugombana, Jumuiya hii itajitahidi kadri iwezekanavyo kupatanisha ili kusimamisha umoja na mapenzi ya Waislamu wote.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (S.W.) Aibariki Jumuiya hii na Muridi wake pamoja na wote wenye kushirikiana nasi na Waislamu kwa jumla. Mwenyezi Mungu (S.W.) Atuepushe na matatizo na yote yaliyo kinyume na madhumuni yetu - **AMIN**.

# II

# KATIBA

# SEHEMU YA KWANZA
## UTAMBULISHO NA UWEZO WA JUMUIYA

### A. JINA

Jina la Jumuiya litakuwa:-

**JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA**

### B. OFISI ZA JUMUIYA

#### (1) MAKAO MAKUU

Makao makuu ya Jumuiya Yatakuwa: Dar es salaam, Kiwanja Nambari 808 Kitalu "D" Mburahati kwa Jongo ,S.L.P.16430 DAR ES SALAAM-TANZANIA.

#### (2). OFISI NDOGO:

Ofisi ndogo za Jumuiya zitakuwa:-

(1) Dar-Es-Salaam;
(2) Arusha;
(3) Zanzibar;
(4) Kigoma;
(5) Musoma;
(6) Mbeya;
(7) Tunduru;
(8) Mtwara;
(9) Dodoma;
(10) Morogoro.
(11) Tabora.

Wakati wowote inapotokea ulazima wa

kufungua Ofisi Ndogo kwa ajili ya kutoa huduma bora zaidi kwa Wana-Jumuiya mahali popote, Ofisi Ndogo inayohusika itawasilisha mapendekezo yake kwa Kamati Kuu, na Kamati Kuu itazingatia mapendekezo hayo na kuidhinisha ikiona inafaa.

## C. AKAUNTI ZA BENKI

Kwa kuanzia Jumuiya itakuwa na Akaunti moja, Dar-Es-Salaam kama ifuatavyo:

**1) DAR-ES-SALAAM:** Account number: 01J/10/276467/00, CRDB AZIKIWE BRANCH DAR ES SALAAM.

Utoaji wa fedha Benki utadhaminiwa na Mlezi, Mwenyekiti, Katibu Mtendaji, Mhasibu Mkuu.

### KUFUNGUA AKAUNTI:

Wakati wowote itakapoonekana kuna haja ya kufungua Akaunti nyingine zaidi pahala popote ili kurahisisha utendaji kwa shughuli za Jumuiya, Kamati Ndogo ya Utendaji itakuwa inao uwezo wa kuongeza Akaunti za Jumuiya kama itakavyoona inafaa.

Utoaji wa fedha Benki utadhaminiwa na waweka saini wawili katika watu wenye nyadhifa za Naibu Mwenyekiti, Naibu Katibu Mtendaji, Mjumbe wa Baraza la Wadhamini na Mhasibu au Mshika Fedha.

## D. UWEZO WA JUMUIYA

Jumuiya itakuwa na mamlaka kamili yenye uwezo ki-Sheria wa kumiliki mali ya aina yoyote inayoondosheka na isiyoondosheka, kununua, kuuza, kuingia katika Mikataba ya aina yoyote na vyombo vingine ili kuendesha shughuli na madhumuni yanayokusudiwa. Hali kadhalika, Jumuiya itakuwa na uwezo ki-Sheria wa kushitaki au kushitakiwa kwa Jina la **Wadhamini wa Jumuiya**.

## E. UANA-JUMUIYA

1. Waislamu wote bila ya kujali rangi au asili wanaweza kuwa Wana-Jumuiya au kuingia katika Jumuiya bila ya ada au kiingilio;
2. Misikiti, Mazawiya, na Vyuo vinaweza kuingizwa na kuwa ndani ya mali za Jumuiya kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Jumuiya baada ya kujaza fomu maalum za maombi na kukubaliwa. (Tazama **Kiambatanisho"B" uk 85).**

# SEHEMU YA PILI

# MADHUMUNI

## A. MADHUMUNI MAKUBWA:

Madhumuni makubwa ya Jumuiya hii yatakuwa ni kuhifadhi, kuimarisha, kukuza, kueneza na kufundisha mwenendo na tabia bora za Kiislamu kama zilivyopokelewa katika Qur'ani na Sunna za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.), na jitihada za Maswahaba na Wanavyuoni waongofu (R.A.) waliokuja baada yao. Katika kufanya hayo, Jumuiya itaanzisha na kutekeleza shughuli mbali mbali kwa lengo la kuwasaidia watu kwa hali na mali ili waweze kuwa na utulivu unaohitajika katika kufanikisha Ibada zao. Hata hivyo, mkazo mkubwa utawekwa kwenye mafunzo kwa vitendo juu ya mwenendo wa maisha ya Kiislamu. Hivyo, Jumuiya hii haitojishughulisha kwa namna yoyote na shughuli zozote za kisiasa, na haitoruhusu, Chuo, Msikiti, Zawiya, Kituo au jina lake kutumiwa na mtu mmoja au kikundi cha watu wakiwa Muridi au wasiwe Muridi katika kufanikisha mambo yao ya kisiasa au ya ki-binafsi. Kwa hiyo, Jumuiya hii inajitenga na haitohusika na mtu au kikundi cha watu

wowote, Wana-Jumuiya au wasiokuwa Wana-Jumuiya watakaofanya hivyo, ikiwa katika pahala pa Jumuiya au penginepo.

## B. ELIMU NA IBADA:

1. Kuendesha shughuli zote za Jumuiya kulingana na mafundisho na miongozo ya Qur'ani na Hadithi za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.).
2. Kuanzisha, kusimamia/ kuongoza na kumiliki Misikiti na Mazawiya ya Qadiriya, popote nchini Tanzania.
3. Kuanzisha, kusimamia/ kuongoza na kumiliki Madrasa, Shule za Kiislamu na Shule za kawaida mahali popote Tanzania.
4. Kuanzisha na kumiliki vitengo vya uchapishaji.
5. Kutafsiri, kuandika na kuchapisha Vitabu vyenye kulingana na Itikadi yetu na maandiko mengine yoyote ya Ki-Dini kwa ajili ya kueneza Elimu ya Kiislamu.
6. Kuinua kiwango cha DINI ya Kiislamu, kwa kuwasomesha Waislamu hapa nchini na nje ya nchi.
7. Kueneza na kuendeleza UISLAMU nchini;

8.Kujishughulisha zaidi na mafunzo, utaratibu na mwenendo wa Twariqa.

9.Kuanzisha,kusimamia, kuhudumia, kumiliki makazi na shule za wasiojiweza, walemavu na mayatima.

## C. AFYA:

1.Kuanzisha, kuendeleza na kumiliki Zahanati pamoja na kutoa huduma mbali mbali za Afya, sambamba na taratibu za Serikali za Tanzania kuhusu mambo hayo.

2.Kueneza huduma za maji safi kwa jamii.

## D. KILIMO:

Kupata na kumiliki ardhi kwa ajili ya Miradi mbali mbali ya

Kilimo na Ufugaji, kulingana na madhumuni ya Jumuiya.

## E. BIASHARA:

Kujishughulisha na Biashara mbali mbali zinazokubaliana na Sharia za Kiislamu na Sheria za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## F. HUDUMA NYINGINEZO:

1.Jumuiya itatoa huduma nyinginezo katika Jamii kwa mujibu wa Sharia za **DINI** na Sheria za Serikali ama kwa kuombwa au inapowajibika Ki-Dini au Ki-Binadamu. Miongoni mwa huduma hizo ni:-

(i) Kuwahudumia Waislamu wanaotaka kwenda Makka kutekeleza Nguzo ya Tano ya Kiislamu ya Hijja.

(ii) Kupokea na kutoa Zawadi, Zaka, Sadaka, Ruzuku, Misaada na Mikopo isiyokuwa na Riba kutoka kwenye Jumuiya za Ki-Dini kama hii, na watu binafsi nje na ndani ya nchi kulingana na Sheria za Serikali.

2. Jumuiya itakuza na kudumisha maelewano na mashirikiano kati ya Jumuiya hii na Jumuiya nyingine yoyote ya Kiislamu, vikundi vya watu au watu binafsi, ikiwa kutoka ndani au nje ya Tanzania kufuatana na misingi ya Qur'ani na Sunna za Bwana Mtume Muhammad (S.A.W.).

3. Jumuiya itawahudumia Mayatima na Vizuka kwa kadri ya uwezo wake.

# SEHEMU YA TATU

## MUUNDO WA JUMUIYA

### A. VIONGOZI WA JUMUIYA

### 1. MLEZI WA JUMUIYA

(a) Atakuwepo Mlezi wa Jumuiya ambaye anapaswa katika maisha yake awe kiigizo kizuri kwa Wana-Jumuiya.

(b) Mlezi wa Jumuiya atakuwepo kwenye nafasi hiyo kutokana na taratibu, desturi, uzoefu, na imani za Twariqa.

(c)Mlezi wa Jumuiya ni lazima awe mwenye sifa zifuatazo:-

i.Mwenye elimu ya kutosha ya Dini;

ii.Mwenye bidii sana ya kumcha Mwenyezi Mungu (S.W);

iii.Muadilifu;

iv. Mwenye busara na hekima;

v. Mwenye kushughulika sana na kazi za Jumuiya;

vi. Mwenye umri usiopungua miaka arobaini (40).

(d) Mlezi wa Jumuiya atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Masheikh na ataweza kuhudhuria Kikao chochote katika vikao vya Jumuiya.

(e) Mlezi ndiye atakuwa muamuzi wa mwisho katika mambo ya Jumuiya na atakuwa na uwezo wa kuzuia azimio lolote lenye muelekeo tofauti na madhumuni ya Jumuiya, litakalokuwa limepitishwa katika vikao vya Jumuiya.

(f) Mlezi wa Jumuiya ndiye atakayeteua Kamati ya Masheikh pamoja na kumteua Naibu Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

(g) Mlezi wa Jumuiya atawateua Wadhamini, Mwenyekiti na Katibu Mtendaji wa Jumuiya pamoja na Wakuu wa Idara. Uteuzi huo utapelekwa kwenye Kikao kinachofuata cha Mkutano Mkuu kwa utambulisho.

(h) Mlezi wa Jumuiya atatembelea Vituo na Mazawiya ya Jumuiya kwa kulingania DINI.

(i) Mlezi wa Jumuiya, kwa kushauriana na Kamati ya Masheikh, atahusika na kutoa Miongozo na Fat-wa za Ki-Dini na Ki-Ibada.

(j) Endapo nafasi ya Mlezi wa Jumuiya itakuwa wazi, nafasi hiyo itajazwa na mtu aliyeusiwa na Mlezi aliyepita kujaza nafasi hiyo. Pasipo wasia, nafasi hiyo itajazwa na Mwanachuoni atakayeteuliwa na Kikao cha pamoja cha Kamati ya Masheikh na Kamati Kuu.

(k) Angalia kiambatanisho "D"uk 97

## 2. MWENYEKITI WA JUMUIYA:

(a) Atakuwepo Mwenyekiti wa Jumuiya atakayeteuliwa na Mlezi wa Jumuiya na kutambulishwa kwenye Mkutano Mkuu.

(b) Mwenyekiti wa Jumuiya ataongoza Vikao vifuatavyo:-

i. Mkutano Mkuu;
ii. Baraza la Wadhamini;
iii. Kamati Kuu.

(c) Mwenyekiti wa Jumuiya atawateua Manaibu Wenyeviti, uteuzi huo utathibitishwa na Baraza la Wadhamini.

(d) Mwenyekiti wa Jumuiya atawateua Manaibu Makatibu Watendaji kwa kushauriana na Katibu Mtendaji. Uteuzi huo utathibitishwa na Baraza la Wadhamini.

(e) Mwenyekiti wa Jumuiya ataweza kuhudhuria kama mshauri, katika Kikao chochote cha Jumuiya mbali na Vikao anavyoviongoza.

(f) Miongoni mwa kazi zake vifungu (b),(c),(d),(e); Mwenyekiti wa Jumuiya atakuwa na jukumu la kutembelea Vituo na Mazawiya, pia yeye ndiye mratibu mkuu wa Hadhara za Ki-Dini, kwa Kalenda za Hadhara za kawaida. (Tazama Kiambatanisho “C”).

## 3. MANAIBU WENYEVITI:

## (Viongozi wa Ofisi Ndogo)

(a) Watakuwepo Manaibu Wenyeviti katika kila Ofisi Ndogo, ambao watateuliwa na Mwenyekiti wa Jumuiya na kuthibitishwa na Baraza la Wadhamini.

(b) Manaibu Wenyeviti wa Jumuiya wataongoza Kamati za Utendaji za Ofisi Ndogo walizokuwepo.

(c) Manaibu Wenyeviti wa Jumuiya wanaweza kuhudhuria kama washauri katika Kikao chochote cha Jumuiya mbali na vikao wanavyoviongoza.

(d) Kwa kushauriana na Mwenyekiti, Manaibu Wenyeviti watawajibika kutembelea Vituo na Mazawiya yaliyo chini ya Ofisi zao Ndogo na kuratibu Hadhara za Ki-Dini.

## 4. KATIBU MTENDAJI:

(a) Atakuwepo Katibu Mtendaji wa Jumuiya atayeteuliwa na Mlezi wa Jumuiya na kutambulishwa kwenye Mkutano Mkuu.

(b) Katibu Mtendaji ndiye atakayekuwa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya. Atawajibika kwenye Kamati Kuu na Baraza la Wadhamini.

(c) Katibu Mtendaji ndiye atakayekuwa:-

i. Katibu wa Mkutano Mkuu;
ii. Katibu wa Kamati ya Masheikh;
iii.Katibu wa Baraza la Wadhamini;
iv. Katibu wa Kamati Kuu;
v. Mwenyekiti wa Sekretarieti;
vi. Mkuu wa Idara ya Uendeshaji.

(d) Akiwa kama Mkuu wa Idara ya Uendeshaji na Mwenyekiti wa Sekretarieti, Katibu Mtendaji atapaswa kusimamia utekelezaji wa Malengo na Shabaha zilizowekwa na Jumuiya.

## 5. MANAIBU MAKATIBU WATENDAJI: Viongozi wa ofisi Ndogo

(a) Kutakuwepo na Manaibu Makatibu Watendaji katika kila Ofisi Ndogo ambao watateuliwa na Mwenyekiti wa Jumuiya kwa kushauriana na Katibu Mtendaji. Uteuzi huu utathibitishwa na Baraza la Wadhamini.

(b) Manaibu Makatibu Watendaji wa Jumuiya watakuwa Makatibu wa Kamati za Utendaji katika Ofisi Ndogo walizoko.

(c) IKiwa Naibu Katibu Mtendaji ye yote hayupo kwa muda, Naibu huyo ataweza kumuachia kazi zake ye yote katika wajumbe kumi waliopo katika Ofisi Ndogo yake, vyenginevyo, Naibu Mwenyekiti wa Ofisi Ndogo hiyo ataweza kumteua yeyote katika wajumbe kumi kushika nafasi hiyo kwa muda.

## 6. WAKUU WA IDARA ;

(a) Pamoja na Idara ya Uendeshaji, zitakuwepo Idara nyengine nne chini ya Sekretarieti kama ifuatavyo:-

i. Fedha na Mipango;
ii. Elimu;
iii. Huduma;
iv. Tiba.

Idara hizi zitaongozwa na Wakuu wa Idara watakaoteuliwa na Mlezi wa Jumuiya na kutambulishwa kwenye Baraza la Wadhamini.

(b) Wakuu wa Idara watapendekeza miundo ya Idara zao kwa Katibu Mtendaji ambaye ataiwasilisha kwenye Kamati Kuu kwa kuthibitishwa.

(c) Wakuu wa Idara watakusanya na kudhibiti taarifa na takwimu muhimu zinazohusu mali za Jumuiya na maendeleo ya shughuli zote za Jumuiya pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi za utekelezaji wa kila siku wa Miradi ya Jumuiya.

(d) Wakuu wa Idara watakuwa na jukumu la kuandaa mipango ya maendeleo na ya uendeshaji wa kila siku wa shughuli zilizo chini ya Idara zao, ikiwa pamoja na Makisio ya Mapato na Matumizi, na kuyawasilisha kwenye Kamati Kuu.

(e) Wakuu wa Idara wataongoza na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote zilizo chini ya Idara zao.

## 7. VIONGOZI WA VITUO:

(a) Kituo kitakuwa chini ya Uenyekiti wa Mwanajumuiya muadilifu na mwenye hekima na busara ambaye anajiheshimu na kuheshimiwa na Wanajumuiya. Awe mwenye umri usiopungua miaka arobaini (40).

(b) Wenyeviti wa Vituo walioko sasa katika Vituo wataendelea na hawatobadilishwa. Iwapo nafasi ya Mwenyekiti wa Kituo itakuwa wazi, Kamati ya Kituo itamteua Mwanajumuiya kujaza nafasi hiyo na kuwasilisha jina lake kwa Kamati Ndogo ya Utendaji ya Ofisi Ndogo inayohusika kwa uthibitisho.

(c) Kituo kitakuwa na Katibu atakayechaguliwa na Mkutano wa Wanajumuiya walioko katika Kituo husika.

(d) Kutakuwa na wajumbe kadri ya kumi, wakiwemo Mwenyekiti na Katibu watakaounda Kamati ya Kituo. Idadi hii inaweza ikazidi au ikapungua kutegemeana na eneo lenyewe. Hakutakuwa na ruhusa ya kumpunguza kiongozi aliyekuwepo tangu zamani.

(e) Kamati za Vituo zitakuwa na jukumu la kusimamia utunzaji wa Mazawiya, Misikiti na

Vyuo vya Jumuiya, na zitatoa taarifa zao kwa Katibu wa Ofisi Ndogo inayohusika kuhusu maendeleo ya shughuli za Jumuiya kwa ujumla, na kuhusu hali halisi ya mali za Jumuiya zilizopo kwenye Vituo vyao na hatua wanazochukuwa kufanikisha hali nzuri wakati wowote.

(f) Hakutakuwa na Kituo katika maeneo yenye Ofisi Ndogo, kama vile Dar-Es-Salaam, Arusha na kadhalika.

(g) Kwa kushirikiana na Kamati za Mazawiya, Kamati za Vituo zitashughulikia ugharimiaji na uendeshaji wa Hadhara zote zinazofanywa Ki-Jumuiya kila mwaka katika Vituo au Mazawiya yao.

## 8. VIONGOZI WA MAZAWIYA:

(a) Zawiya litakuwa chini ya Uenyekiti wa Mwenyekiti muadilifu na mwenye hekima na busara ambaye anajiheshimu na kuheshimiwa na Wanajumuiya walioko kwenye Zawiya lake. Kiongozi huyo atatakiwa awe ana umri usiopungua miaka thelathini (30).

(b) Wenyeviti wa Mazawiya walioko sasa wataendelea na hawatobadilishwa. Iwapo nafasi ya Mwenyekiti wa Zawiya itakuwa wazi, Kamati ya Zawiya itamteua Mwanajumuiya wa kujaza nafasi hiyo. Mteuliwa huyo atathibitishwa na Kamati Ndogo ya Utendaji ya Ofisi Ndogo

inayohusika.

(c) Zawiya litakuwa na Katibu atakayechaguliwa na Mkutano wa Wanajumuiya walioko katika Zawiya hilo.

(d) Zawiya litakuwa na Kamati yenye wajumbe watano wakiwemo Mwenyekiti na Katibu. Idadi hii inaweza ikazidi kutegemeana na Zawiya lenyewe. Hakutakuwa na ruhusa ya kumpunguza Kiongozi yeyote ambaye anajulikana kuwa kiongozi tangu zamani.

(e)Kamati za Mazawiya zitakuwa na jukumu la kusimamia Uendeshaji wa Ibada na Mafunzo ya Ki-Dini kwa ujumla katika Mazawiya, Misikiti na Vyuo vya Jumuiya. Mafunzo haya yatatia mkazo kwenye Elimu na Malezi ya Ki-Twariqa.

(f)Kamati za Mazawiya zitakuwa pia na jukumu la kusimamia na kuhakikisha Walimu, Makhalifa na Masheikh wanaosomesha na kuongoza Ibada wanapata mahitaji ya lazima kwa maisha yao na familia zao kwa kiasi cha kutosha kuwawezesha kuendelea na kazi zao bila matatizo makubwa.

(g)Kwa kushirikiana na Kamati za Vituo, Kamati za Mazawiya zitashughulikia ugharimiaji na uendeshaji wa Hadhara zote zinazofanywa Ki-Jumuiya kila mwaka katika Mazawiya au vituo vyao.

(h) Wenyeviti na Makatibu wa Mazawiya wataitisha Mikutano ya kawaida ya Mazawiya mara mbili kwa mwaka. Ki-msingi, Hadhara zote binafsi zinazoendeshwa na Jumuiya zitagharamiwa na kusimamiwa na wanaohusika. Hata hivyo, uendeshaji wa Hadhara hizo utafanywa kufuatana na miongozo ya Jumuiya. Wanajumuiya binafsi yao wanahimizwa wawasaidie wenye Hadhara katika michango na usimamizi wa Hadhara za wenzao ili kuongeza udugu na mapenzi ya Kiislamu.

## B. VIKAO VYA JUMUIYA

### 1. MKUTANO MKUU WA JUMUIYA:

(a) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya utakaoitishwa na Mwenyekiti wa Jumuiya kupitia kwa Katibu Mtendaji ambao utahudhuriwa na Wanajumuiya wote watakaoweza. Lakini lazima Mkutano Mkuu uhudhuriwe na zaidi ya nusu ya Wadhamini wote, na nusu ya Wajumbe wa Kamati ya Masheikh ili Kikao hicho kipate uhalali. Kwa maana hii wadhamini wanaohudhuria Vikao vya Mkutano Mkuu itabidi wanakiliwe majina yao. Endapo idadi yao itapungua chini ya idadi inayotakiwa kuhalalisha Mkutano, Kikao hicho kitageuzwa kuwa Semina ya Mafunzo ya Dini.

(b) Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu atakuwa Mwenyekiti wa Jumuiya au mmoja kati ya Manaibu wake.

(c) Katibu wa Mkutano Mkuu atakuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya au mmoja kati ya Manaibu wake.

(d) Mkutano Mkuu wa kawaida utafanyika mara moja katika kipindi cha miaka mitatu.

(e) Patakuwa na Mkutano Mkuu Maalum utakaoitishwa na Mwenyekiti wa Jumuiya kwa kushauriana na Mlezi na Katibu Mtendaji wa Jumuiya kujadili mambo ya dharura yanayohitaji kibali cha Mkutano Mkuu.

(f) Mkutano Mkuu utakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuwatambulisha Wadhamini, Mwenyekiti na Katibu Mtendaji wa Jumuiya, pamoja na Wakuu wa Idara;

ii. Kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Jumuiya;

iii. Kujadili na kupitisha Sera mbali mbali za Jumuiya;

iv. Kujadili na kuthibitisha mapendekezo ya marekebisho na mabadiliko ya Katiba.

## 2. KAMATI YA MASHEIKH:

(a) Kutakuwa na Kamati ya Masheikh itakayojumuisha Masheikh wasiopungua watano

na wasiozidi tisa ambao watateuliwa na Mlezi wa Jumuiya.

(b) Mwenyekiti wa Kamati ya Masheikh atakuwa ni Mlezi wa Jumuiya, ambaye atamteua Naibu Mwenyekiti wa Kamati hii.

(c) Katibu wa Kamati ya Masheikh atakuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya au mmoja wa Manaibu wake. Ikiwa wote hawapo, Kamati itamteua mmoja miongoni mwao kuwa Katibu wa muda.

Hata hivyo, Katibu Mtendaji au yeyote miongoni mwa manaibu wake hawatokuwa wajumbe wa Kamati ya Masheikh isipokuwa kama wameteuliwa na Mlezi.

(d) Kamati ya Masheikh itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Itatoa miongozo yote kwa Jumuiya kulingana na Sharia za Kiislamu, na adabu za Twariqa.

ii. Wajumbe wa Kamati ya Masheikh watatakiwa kutembelea Vituo na Mazawiya ili kuendeleza malezi ya Ki-Twariqa.

iii. Kamati itakuwa ndiyo mshauri mkuu wa Jumuiya;

iv. Kamati ya Masheikh itaweza kualika Masheikh wowote kutoka popote Duniani ili kufanikisha shughuli za Jumuiya.

v. Kamati itawajibika kupeleka Wajumbe

wake katika Vikao vya Mkutano Mkuu, Baraza la Wadhamini, Kamati Kuu, Sekretarieti na Kamati za Utendaji za Ofisi Ndogo za Jumuiya.

vi. Kamati ya Masheikh itakuwa ikikutana wakati wowote inapohitajika.

## 3. BARAZA LA WADHAMINI:

(a) Kutakuwa na Baraza la Wadhamini litakalokuwa na wajumbe wasiozidi wanane (8).

(b) Baraza la Wadhamini litateuliwa na Mlezi na kutambulishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Jumuiya.

(c) Itakapokuwa nafasi ya Mjumbe wa Baraza la Wadhamini iko wazi kwa dharura yoyote, nafasi hiyo itajazwa na Mjumbe mwengine atakaye teuliwa na Mlezi (R.A) na jina lake kupelekwa kwa Kabidhi Wasii.

(d) Mwenyekiti wa Jumuiya atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini, na Katibu Mtendaji wa Jumuiya atakuwa ndiye Katibu wa Baraza la Wadhamini. Iwapo wote hawapo, Baraza litachagua Mwenyekiti au Katibu wa muda miongoni mwao.

(e) Mjumbe wa Baraza la Wadhamini atatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

i. Muislamu muadilifu.

ii.Mwenye umri usiopungua miaka thelathini na tano (35).

iii.Mwenye akili timamu.

iv.Mwenye busara na hekima, mwaminifu, mtulivu na mwenye tabia nzuri.

(f) Baraza la Wadhamini litakuwa na kazi zifuatazo:-

i.Litawajibika na usimamizi wa Mipango na Kanuni za Jumuiya pamoja na utekelezaji wake. Kwa ujumla, shughuli zote za Jumuiya zinazohusu kununua, kuuza na kuingia kwenye Mikataba zitasimamiwa na Baraza la Wadhamini.

ii. Litachambua na kutathmini Miradi na shughuli za kimaendeleo za Jumuiya kabla ya kuiwasilisha kwenye Kikao cha Mkutano Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.

iii. Litapokea na kuthibitisha majina ya Wajumbe wa Sekretarieti na Kamati Ndogo za Utendaji. Wajumbe hao ni lazima wawe ni Wanajumuiya.

iv.Litathibitisha uteuzi wa Manaibu Wenyeviti na Manaibu Makatibu Watendaji.

(g) **Baraza la Wadhamini litamiliki mali zote za Jumuiya na litaweza kushitaki au kushitakiwa kwa niaba ya Jumuiya.**

(h) Baraza la Wadhamini litakutana mara moja kwa mwaka au kila itapohitajika kwa idhini ya Mwenyekiti wa Jumuiya. Ili Kikao chake kiwe halali, ni lazima kihudhuriwe na zaidi ya nusu ya Wadhamini wote, pamoja na wajumbe wa

Kamati ya Masheikh wasiopungua wawili.

Baraza la Wadhamini litaendesha na kutekeleza shughuli zake zote kwa kushauriana na Kamati ya Masheikh na kamati kuu.

## 4. KAMATI KUU:

Kutakuwepo na kamati kuu itakayokuwa na Wajumbe kam ifuatavyo:-

i. Mwenyekiti wa Jumuiya;
ii. Manaibu wote wa Mwenyekiti (ofisi ndogo).
iii. Katibu Mtendaji wa Jumuiya.
iv. Manaibu wote wa Katibu Mtendaji.
v. Wakuu wa Idara zote za Jumuiya.
vi. Angalau Mjumbe mmoja au zaidi wa Kamati ya Masheikh.

(b)Kamati Kuu itakuwa ndiyo mshauri mkuu wa Baraza la Wadhamini.

(c) Kamati Kuu itakuwa na kazi zifuatazo:-

i.Kuthibitisha Miundo ya Idara zote.
ii. Kupokea na kuthibitisha taarifa za Makisio ya Mapato na Matumizi ya Jumuiya.
iii.Kupokea na kupitisha mapendekezo ya kuanzisha Ofisi Ndogo mpya.
iv. Kuandaa mapendekezo ya Marekebisho au Mabadiliko ya Katiba kwa kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu.
v. Kushughulikia mambo yote ya dharura.

(d) Kamati Kuu itakutana wakati wowote itapohitajika chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wa Jumuiya au mmoja wa Manaibu wake. Katibu Mtendaji ndiye atakayekuwa Katibu wa Kamati Kuu au mmoja wa Manaibu wake.

(e) Uhalali wa Maamuzi ya Kamati Kuu utapatikana kwa kuhudhuriwa na Wajumbe wanne kama ifuatavyo:-

i.Mwenyekiti wa Jumuiya au mmoja wa Manaibu wake.

ii.Katibu Mtendaji au mmoja wa Manaibu wake.

iii.Mmoja wa Wakuu wa Idara za Jumuiya.

iv.Mjumbe mmoja kutoka Kamati ya Masheikh.

## 5. SEKRETARIETI:

(a) Kutakuwepo na Sekretarieti ambayo ndiyo itakayokuwa Kamati ya Utendaji ya Baraza la Wadhamini. Kamati hii itaongozwa na Katibu Mtendaji wa Jumuiya. Muundo wa Sekretarieti umewekwa kwenye Kiambatanisho "E"uk 100.

(b) Wajumbe wa Sekretarieti watakuwa kama ifuatavyo:-

i. Katibu Mtendaji (Mwenyekiti).

ii.Mjumbe wa Kamati ya Masheikh.

iii.Manaibu wa Katibu Mtendaji.

iv. Wakuu wa Idara za Jumuiya;

v. Mjumbe mmoja kutoka kila Ofisi Ndogo.

vi. Mhasibu Mkuu wa Jumuiya.

(c) Katibu Mtendaji atamteua mmoja wa Manaibu wake kuwa Katibu wa Vikao vya Sekretarieti. Katibu huyo anaweza kubadilika katika Vikao mbali mbali.

(d) Kwa idhini na kwa niaba ya Baraza la Wadhamini wa Jumuiya, Sekretarieti itashughulikia mambo yafuatayo:-

i. Kukusanya michango na misaada, kuajiri, kuingia katika mikataba, kuuza na kununua. Kwa ujumla kusimamia shughuli zote za Jumuiya kama zilivyoelezwa katika Katiba hii.

ii. Kusimamia shughuli za maandishi na uchapishaji wa vitabu na majarida ya Ki-Dini.

iii. Kuhudumia Vikao vya Jumuiya kama vilivyoelezwa katika Katiba hii.

iv. Kushughulikia safari za Viongozi wa Jumuiya na wageni wa Jumuiya.

v. Kusimamia Ujenzi na Ukarabati wa Mazawiya, Misikiti, Vyuo na majengo mengine ya Jumuiya.

vi. Kuandaa Kanuni za Utumishi na Uendeshaji wa shughuli za Jumuiya.

vii.Sekretarieti itakuwa inakutana mara mbili kwa mwaka katika Vikao vya kawaida, itakutana mara nyengine nyingi kama itakavyohitajika.

## 6. KAMATI ZA UTENDAJI ZA OFISI NDOGO:

(a) Zitakuwepo Kamati za Utendaji za Ofisi Ndogo zenye wajumbe wasiozidi kumi kila moja.

(b) Wajumbe wa Kamati ndogo za Utendaji watakuwa wafuatao:-

i. Naibu Mwenyekiti wa Jumuiya atakuwa ndiye Mwenyekiti.

ii.Naibu Katibu Mtendaji ndiye atakuwa Katibu;

(c) Ofisi ndogo za Jumuiya na Kamati zake za Utendaji zitahudumia na kushughulikia kazi zote za Vituo na Mazawiya yaliyoko katika maeneo yao.

(d) Kamati za Utendaji za Ofisi Ndogo zitakuwa na kazi zifuatazo:-

i. Kusimamia utendaji kazi za Jumuiya za siku hadi siku kwa niaba ya Sekreterieti.

ii. Kusimamia ukusanyaji na udhibiti wa fedha za Jumuiya na zinazotokana na michango, sadaka, misaada, mikopo, na kodi zinazotokana na mali ya Jumuiya.

iii. Kuwathibitisha Wenyeviti wa Mazawiya.

(e) Kamati za Utendaji za Ofisi Ndogo zitakuwa zinakutana mara nne kwa mwaka au wakati wowote zinapohitajika.

(f) Kamati ndogo za Utendaji zitapeleka taarifa zao kwenye Sekretarieti.

# SEHEMU YA NNE
## MENGINEYO

### A. ALAMA YA JUMUIYA:

Kutakuweko na nembo au alama rasmi ya Jumuiya ambayo itakuwa ni mchoro wenye alama ya Nyota na Mwezi.

### B. MUHURI:

1. Patakuwepo na Muhuri wa Jumuiya (SEAL) utakaosomeka: "JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA".
2. Patakuwepo na Muhuri mwengine (Rubber Stamp) utakaosomeka: "JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA" na utakaotumika kwa nyaraka zote zitakazotiwa saini kwa niaba ya Jumuiya. Muhuri huu utaonyesha anuani kamili ya Jumuiya.

### C. VITAMBULISHO:

1. Kwa ajili ya utambulisho, Mwanajumuiya ataweza kupewa kitambulisho cha Jumuiya.
2. Mwanajumuiya atalazimika kulipia sehemu ya gharama za uchapishaji kwa kadri itakavyopangwa na Jumuiya.

## D. KUACHA UONGOZI:

Kiongozi yeyote wa Jumuiya ataacha kuwa katika wadhifa wake kwa sababu zifuatazo:-

1. Akifariki Dunia.
2. Akipata maradhi ya akili yasiyotibika (Mwenyezi Mungu (S.W.) Amkinge kila Muislamu**- AMINA**).
3. Akiacha Uislamu (Mwenyezi Mungu (S.W.) Atulinde Waislamu wote**- AMINA**).
4. Akijiuzulu Mwenyewe.
5. Akihama nchini moja kwa moja.

## E. KUHAMA:

Kiongozi wa Jumuiya anapohama moja kwa moja kutoka eneo la Kituo chake, nafasi yake itajazwa kwa kufuata taratibu za Jumuiya. Lakini yeye ataendelea kupewa heshima ile ile ya Uongozi na kushirikishwa katika Uongozi wa Kituo cha eneo alilohamia.

## F. UHALALI WA VIKAO VYA JUMUIYA (QUORUM):

Mikutano yote ya Jumuiya ili iwe halali, ni lazima wakutane nusu au zaidi ya nusu ya Wajumbe wa Kikao hicho, isipokuwa ilipoelezwa vyenginevyo.

## G. UTATUZI WA MATATIZO:

1.Matatizo yote yatakayojitokeza kati ya Wanajumuiya yatashughulikiwa tu na Jumuiya yenyewe kwa utaratibu ufuatao:-

i. Viongozi wa Zawiya.
ii. Viongozi wa Kituo.
iii. Viongozi wa Kamati Ndogo za Utendaji.
iv. Mwenyekiti wa Jumuiya.
v. Mlezi wa Jumuiya.

2. Iwapo Mwanajumuiya ana matatizo na mtu asiyekuwa Mwanajumuiya, Jumuiya itajitahidi kusuluhisha kadri ya uwezo wake. Ikishindikana itatoa ruhusa jambo hilo lishughulikiwe nje ya Jumuiya.

## H. KUSIMAMISHWA UONGOZI:

Kiongozi yeyote atakayekwenda kinyume cha utaratibu wa Maadili (Madhumuni) ya Jumuiya atasimamishwa uongozi. Iwapo katika kipindi cha mwaka mmoja atakuwa hajajirekebisha, basi atateuliwa Msaidizi katika shughuli zake.

## I. MALIPO:

Masheikh, Wadhamini, na Watumishi wote wa Jumuiya wataweza kulipwa mishahara kama inavyostahili hapo hali ya Jumuiya itakapokuwa nzuri Ki-fedha. Kwa sasa shughuli zote za Jumuiya zitaendeshwa kwa kujitolea.

## J. MAREKEBISHO YA KATIBA:

Katiba hii inaweza kurekebishwa kwa kuongezwa au kupunguzwa kifungu au sehemu ya Maandiko na Mkutano Mkuu wa Jumuiya na kukubaliwa na zaidi ya nusu ya Wajumbe waliohudhuria.

## K. BENDERA

Jumuiya Zawiyatul Qadiriya Tanzania inayo Bendera yenye Rangi tatu ambazo ni Nyeupe, Nyekundu na Kijani. Rangi Nyeupe hiyo ndiyo huishikilia Bendera katika mti wake. Rangi Nyekundu na kijani hizo hupepea, yakiwepo maandishi maalumu kwa uzi mweupe katika Rangi ya Kijani.

## MATUMIZI YA BENDERA

Bendera itapepea katika Mazawiya (vituo), katika Hadhara,katika misiba na katika misafara ya Kidini.

# SEHEMU YA TANO

## A. UTHIBITISHO (CERTIFICATION)

Sisi Wadhamini wa Jumuiya Zawiyatul Qadiriya Tanzania tuliotajwa hapa chini tunathibitisha kuwa, Kanuni hizi ni sahihi kwa upeo wa imani zetu, kama zilivyotengenezwa na kupitishwa katika Kikao cha Mkutano Mkuu wa Nne wa Jumuiya uliofanyika Dar-Es-Salaam tarehe 9/7/2006.

| NA | KITUO | JINA | SAINI |
|---|---|---|---|
| 1. | ZANZIBAR | Seyyid Othuman AbdulQaadir | |
| 2. | DAR-ES-SALAAM. | Sheikh Swaleh Ahmed Jouban | |
| 3. | DAR-ES-SALAAM. | Sheikh Yusuff Bakari | |
| 4. | DAR-ES-SALAAM. | Al-haj Ibrahim Ally | |
| 5. | DAR-ES-SALAAM. | Sheikh Haji Mhina | |
| 6. | ARUSHA | Al-haji Hamisi .S. Migire | |
| 7. | KIGOMA | Sheikh Juma Ibrahim Mtale | |
| 8. | PWANI | Sheikh Twalib Sematole | |

# B. VIAMBATANISHO

## 1. KIAMBATANISHO "A"

## SILSILAH YA TWARIQATUL QADIRIYA UWEISIYYAH MAPOKEZI YA MKONO KWA MKONO KUANZIA KWA BWANA MTUME MUHAMMAD (S.A.W.)

1. **SAYYIDINA MUHAMMAD IBN ABDILLAH (S.A.W.)**
2. SAYYIDINA ALI BIN ABI TWALIB (K.W.)
3. SAYYID HASSAN EL-BISRIY (R.A.)
4. SAYYID HABIB EL-AJAMIY (R.A.)
5. SAYYID DAWOOD AT-TWAIY (R.A.)
6. SAYYID MAARUF EL-KARKHIY (R.A.)
7. SAYYID SIRRIY ES-SAQTIY (R.A.)
8. SAYYID ABUL-QASSIM JUNAYDI EL-BAGHDADIY (R.A.)
9. SAYYID ABUBAKAR ASH-SHIBLIY (R.A.)
10. SAYYID ABUL-FADH-LI ABDULWAHID ET-TAMIMY (R.A.
11. SAYYID ABUL-FARAJI ET-TWARSUSIY (R.A.)
12. SAYYID ABUL-HASSAN-EL-HIKARIY (R.A.)
13. SHEIKH ABU-SAIDIL MUBARAK EL-MAKHZUMIY (R.A.)
14. **SAYYID ABDUL QAADIRI EL-JAYLANIY (K.S.)**
15. SAYYID ABDUL AZZIZ (R.A.)
16. SAYYID MUHAMMAD EL-HITAKY (R.A.)
17. SAYYID SHAMSUDDIN BIN MUHAMMAD (R.A.)
18. SAYYID SHARAFUDDIN BIN SHAMSUDDIN (R.A.)
19. SAYYID ZAYNUDDIN BIN SHARAFUDDIN (R.A.)
20. SAYYID WALIYYDDIN BIN ZAYNUDDIN (R.A.)
21. SAYYID NURUDDIN BIN WALIYYIDDIN (R.A.)
22. SAYYID YAHYA BIN NURUDDIN (R.A.)
23. SAYYID ABUBAKARI BIN YAHAYA (R.A.)
24. SAYYID HISAMUDDIN (R.A.)

25.SAYYID MUHAMMMAD DAR-WEISH (R.A.)
26.SAYYID NURUDDIN BIN MUHAMMAD (R.A.)
27.SAYYID ABDULWAHHAB BIN NURUDDIN (R.A.)
28.SAYYID ISMAIL BIN ABDULWAHHAB (R.A.)
29.SAYYID ABUBAKARI BIN ISMAIL (R.A.)
30.SAYYID ABDULQADIRY EL-QADIRY (R.A.)
31.SAYYID ALI EL-QADIRY (R.A.)
32.SAYYID MUSTAFA BIN SALMAN EL-QADIRY (R.A.)
**33.SHEIKH UWEIS BIN MUHAMMAD EL-QADIRY (R.A.)**
34.SAYYID OMAR QULLATAYNI EL-QADIRY (R.A.)
35.SHEIKH ABDALLA BIN AHMAD EL-QADIRY (R.A.)
**36.SHEIKH MUHAMMAD NASSOR ABDULLA EL-QADIRY (R.A.)**

## 2. KIAMBATANISHO "B"

**JZQ 1**

**JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA**

**P. O. BOX 16430, DAR-ES-SALAAM**

KWA KATIBU MTENDAJI

JUMUIYA ZAWIYATUL QADIRIYA TANZANIA

## MAOMBI YA MALI ZINAZOKABIDHIWA JUMUIYA

1. Jina la Mwombaji/ Waombaji (M/Kiti/ Imamu/Katibu ............................................................
2. Anuani: S.L.P ....... Simu:........ Mji..........
3. Maelezo kuhusu ombi:

(a) Kinachoombewa:- Zawiya/ Msikiti/ Chuo/ Kiwanja/ au ...........................

Plot No ........ Block No........ Mtaa/ Kitongoji/Kijiji/ Shehea .............. Kata ................. Tarafa ............... Wilaya .................... Mkoa ..........................

(b) Ukubwa ..........................

Mipaka:-

Kaskazini .......... Kusini …………… Mashariki ................. Magharibi ....................

(c) Zawiya/ Msikiti/Chuo/ Kiwanja/ au ………… hakikuandikishwa na wala hakipo chini ya uongozi wa Jumuiya yoyote.

4. Viongozi/Wadhamini wa watoaji.

| **Jina** | **Sahihi** |
|---|---|
| 1) ........................................................ | ............ |
| 2) ........................................................ | ............ |
| 3) ........................................................ | ............ |
| 4) ........................................................ | ............ |
| 5) ........................................................ | ............ |
| 6) ........................................................ | ............ |
| 7} ........................................................ | ............ |
| 8) ........................................................ | ............ |
| 9) ........................................................ | ............ |
| 10) ........................................................ | ............ |

**5. UTHIBITISHO:**

Mimi/Sisi tunathibitisha kuwa maelezo yote yaliyotolewa na muhusika/ wahusika ambao tunawafahamu ni sahihi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/ Sheha au Mwenyekiti wa MKitongoji au Katibu Mtendaji au Katibu Tarafa/ Diwani.......

1. Mwenyekiti/Katibu Baraza la Ardhi la Kijiji.

JINA ………………………………………..

Saini na Muhuri......................

Tare he ..../.../…….

2. Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/ Sheha au Kitongoji au Katibu Mtendaji au Katibu Tarafa/ Diwani

JINA .....................

Saini na Muhuri .......................
Tare he ..../..../.....

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU:**

Fomu Na. JZQ.1 ya tarehe .......... kuhusu ombi la ............ limekubaliwa/limekataliwa katika kikao cha tarehe ............ kwa sababu zifuatazo:
..........................................................................................
..........................................................................................

Saini ya aliyepitisha ...............

Katibu Mtendaji .....................

**NB:** Nakala za Hati/Vielelezo vya kuthibitisha haki za kumiliki Kama vipo viambatishwe.

# 3. KIAMBATANISHO "C"
## KALENDA YA HADHARA ZA QADIRIYA KATIKA MWAKA

| MFUNGUO | TAREHE | HADHARA | MAHALA |
|---|---|---|---|
| NNE | 1 | DUA KUOMBEA MWAKA MPYA | NCHINI KOTE |
| | 9 | YAUMUN ASHURA | KWA SHEIKH ABDULKARIM (LINDI) |
| | 10 | YAUMUN ASHURA | KILA ZAWIYA |
| | 11 | HADHARA | KILWA SINGINO |
| | 13 | SHEIKH OMAR FARAHANI (R.A.) | KILWA KIVINJE |
| | 13 | SHEIKH OMAR FARAHANI (R.A.) | BUNJU BAGAMOYO |
| | 13 | SHEIKH MUHAMMAD NASSOR ABDULLA EL QADIRIY (RA) | BALADUL AMINI MBURAHATI DAR-ES-SALAAM |
| | JUMA PILI INAYOFUATA | SHEIKH MUHAMMAD NASSOR ABDULLA EL QADIRIY (RA) | BALADUL AMINI ZANZIBAR |
| | ,, | ,, | KALANJE TUNDURU |
| | 17 | SHEIKH ABDALLA HAMADI (RA) | KIGOMBE, TANGA |
| | 24 | SHEIKH SULEIMAN EL-ALAWY (R.A.) | BUGURUNI |
| | 28 | HADHARA | ZAWIYANI MABAWA TANGA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 29 | HADHARA | KWA BWANA MHINA TANGA |
| TANO | 5 | BI AMDA (MAMA YAKE SHEIKH MUHAMMAD NASSOR ABDULLA EL-QADIRY) | BALADUL-AMIN, MANZESE, DAR-ES-SALAAM |
| | JUMAMOSI YA PILI | HADHARA | NDUNDU KIVUKONI, RUFIJI |
| | " | HADHARA | BAGAMOYO MJINI |
| | JUMAMOSI YA TATU | HADHARA | MWANANYAMALA KISIWANI DAR-ES-SALAAM |
| | JUMAMOSI YA MWISHO | SHEIKH SUFI (R.A) | CHAMWINO MOROGORO |
| SITA | 7 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | KILWA MANDAWA |
| | 11 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | KILWA KIVINJE |
| | 13 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | KIGOMA |
| | 11 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | KIBAHA |
| | 13 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | MINGOMBE KISIJU |
| | 15 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | MLANDIZI |
| | 16 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | TABORA |
| | 18, 19-20 | SHEIKH UWEIS | MUSOMA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | AHMAD (R.A.) | |
| | 22-23 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | MWANZA |
| | 22 | SHEIKH UWEISU BIN AHMAD (R.A) | MATEMANGA TUNDURU |
| | 25 | MAULIDI YA SEYYIDINA MUHAMMAD (S.A.W.) | DODOMA |
| | 26, 27-28 | SHEIKH UWEIS AHMAD (R.A.) | BALADUL-AMIN MBURAHATI DAR |
| SABA | 3 | SHEIKH ALI OMAR | MKAMBA KWA SHEIKH IMAMU MKAMBA |
| | 10 | SEYYID ABDULQADIR JEILANY (Q.S) | (1) KINONDONI |
| | 10 | " | (2) KIPERA MOROGORO |
| | 10 | " | (3) TUNDURU MJINI |
| | 11 | " | KWA MSISI TANGA |
| | 17 | SEYYID ABDULQADIR JEILANY (Q.S.) | IKWIRIRI, RUFIJI |
| | 20 | ZIARA KUU YA SEYYID ABDULQADIR JEILANY (K.S.) | KINONDONI |
| | 20 | ,, | KADEWELE TUNDURU |
| | 20 | " | ARUSHA |
| | JUMA MOSI YA TATU | SHEIKH ABDALLAH HAMADI (R.A) | VIBAMBANI NA TANGA MJINI. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 24 | SHEIKH ABDALLAH HAMMAD (R.A.) | BINGA, KISIJU |
| | JUMAMOSI YA MWISHO | “ | KIGAMBONI |
| NANE | 7 | SHEIKH MUHAMMAD NASSOR ABDULLA EL QADIRIY (RA) | SINGIDA MJINI |
| | 8 | HADHARA | KIJIJINI DIAGWA |
| | 9 | HADHARA | MWAKITI/MVAE |
| | 10 | HADHARA | KITITIMO |
| | 11 | HADHARA | IKUNGI/MATARE / MANG'ONYI |
| | 12 | HADHARA | UNYANKINDI |
| | 13 | HADHARA | SEPUKA |
| | 14 | ZIARA | ZANZIBAR |
| | 16 | SHEIKH MUSSA KASSIM (R.A) | MZURI KAJA MAKUNDUCHI ZANZIBAR |
| | JUMA MOSI YA TATU | SHEIKH ABDALLAH HAMADI - MOMBASA | MOMBASA, LAMU, SIYU, PATE NA MALINDI |
| TISA | 8 | HADHARA | MLINGANO, TANGA |
| | 10 | SEYYIDINA ABUBAKAR(R.A.) UFUNGUZI | TANDIKA DARES-SALAAM |
| | 11 | “ | “ |
| | 12 | HADHARA KUU YA SEYYIDINA ABUUBAKAR (R.A) | TANDIKA |
| | 12 | “ | (2) KIRARE |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | TANGA |
| | 16 | SHEIKH MUSSA BIN UWEIS (R.A.) | MBUTU, KIGAMBONI |
| RAJAB | 7 | IMAAMU SHAFII (R.A.) | KILWA MANDAWA |
| | 8 | SHEIKH SHEGO UWEISU (R.A.) | KINONDONI |
| | 9 | SEYYID ABDULQADIR JAILANIY (Q.S.) | KILWA MASOKO |
| | 11 | SHEIKH OMAR FARHAN (R.A) | KILWA KIVINJE |
| | 12 | HADHARA | KILWA SINGINO |
| | 14 | HADHARA | MAZAWIYA YOTE |
| | 14 | SEYYID AHMAD (R.A) | KILWA PANDE |
| | 21 | SEYYID SALMIN BIN SAIDI | BALADUL AMINI DAR-ES-SALAAM |
| | 29 | IMAM SHAAFY (R.A.) | KEKO, DAR-ES-SALAAM |
| SHABAN | 14 | KUADHIMISHA NISFU SHABAN | MAZAWIYA YOTE |
| | 17 | SEYYID HASSAN (MTUME CHIMO) | MKAMBA, MBURANI |
| | 24 | SHEIKH ISMAIL JUMAA | MPAFU |
| | 28 | SEYYID ABDULQADIR JEILANY (Q.S.) KUZALIWA | TANDALE |
| | 29 | SEYYID ABDULQADIR JEILANY (Q.S.) KUZALIWA | KILWA KIVINJE |
| RAMADHANI | 10 | KUFUTRU KWA SHEIKH MUHAMMAD | BALADUL AMIN MANZESE |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | NASSOR ABDULLA EL-QADIRY KWA BI MTUMWA (R.A) | |
| | 16 | KUADHIMISHA BADRI | (1) KIGAMBONI DAR-ES-SALAAM |
| | 17 | KUADHIMISHA BADRI | MWANANYAMA LA |
| | 20-30 | ITIKAFU | MAZAWIYA YOTE INAKOFANYIKA ITIKAFU |
| | 21 | SEYYIDINA ALLY (KW) | ITIKAFU ZOTE |
| | 24 | WAZEE WA SH. MUHAMMA .N. (R.A) NA MASHEIKH WOTE (R.A) | MAZAWIYA YOTE INAKOFANYIKA ITIKAFU |
| | 26 | IHIYAU LAILATULKADIR | ITIKAFU ZOTE |
| | 28 | DUA YA WASAIDIZI WA ITIKAFU | ITIKAFU ZOTE |
| | 29 | IHIYAU AKHER LAILATI RAMADHANI | ITIKAFU ZOTE |
| MOSI | 7 | HADHARA | KOKOBO KISIJU |
| PILI | 20 | (1) SHEIKH THINEY (RA) | KIPERA |
| | | (2) SHEIKH ISSA (RA) | MOROGORO |
| TATU | 5 | HAULI YA WAZAZI WA BW. ALI OMAR SEKO | MTONI AZIMIO DAR-ES-SALAAM |
| | 7 | (1)IHIYAU TAREHE 7 USIKU KUAMKIA TAREHE 8 | KILA ZAWIYA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 7 | (2) KUWAREHEMU MASHEIKH WOTE | KILA ZAWIYA |
| | 8 | IHIYAU/YUAUMI TARAWIA | KILA ZAWIYA |
| | 9 | IHIYAU/YAUMI ARAFA (SAUM) | KILA ZAWIYA |
| | 9 | IHYAU LAILATIL IDI | MAZAWIYA YOTE |
| | 17 | SEYYIDINA ATHUMAN (RA) | KWA SHEIKH ALI MPITA MANZESE DAR-ES-SALAAM |
| | 30 | SEYYIDINA OMAR (RA) | MBAGALA KWA SHEIKH ABDALLAH (R.A) |
| **ZIFUATAZO NI HADHARA ZENYE TAREHE ZA KIZUNGU** | | | |
| MWEZI | TAREHE | HADHARA | MAHALA |
| JULAI-AGOSTI | 28-12 | BUKOBA, MASAKA, JINJA NA SOROTI | KAGERA NA UGANDA. |
| OCTOBA | 12 | HADHARA | QASHI |
| | | | |
| OCTOBA | 13 | SH. MUHAMMAD .N.ABDULLA (R.A) | BUKULU |
| | 14 | HADHARA | KONDOA MJINI |
| | 15 | HADHARA | KWA MAFUNCHI |
| | 16 | HADHARA | THAWI NJIA PANDA |
| | 17 | HADHARA | THAWI BOOLO |
| | 18 | HADHARA | SIROP |
| | 19 | HADHARA | ENDASAKI |
| | 20 | SH. MUHAMMAD .N. ABDULLA (R.A) | BABATI |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 21 | HADHARA | GICHAMEDA |
| | 22 | SEY. ABDULQADIR JAILANI (QS) | ARUSHA |
| | 23 | HADHARA | MOSHI |
| | 24 | HADHARA | KIRUANI |
| | 25 | HADHARA | KIHURIO |

**ANGALIA**: 1.Muridi na Waislamu wote wanapofikwa na misiba Maiti wao wafanyiwe Tahlili (wakipenda)

2. Ni jambo bora kabisa kwa kila Muislamu kujitahidi kuwaombea wazee wake au ndugu zake waliokwisha kufa ikiwezekana mara mbili, tatu au zaidi kila mwaka.

3. Mwaka wa Kiislamu unaanzia tarehe mosi mfungo nne (Muharram). Hivyo ni muhimu kwa Waislamu wote popote walipo kufanya Dua ya kheri kwa kuombea mwaka mpya.

4. Tarehe zifuatazo ni muhimu sana (pengine ni wajibu) kwa Waislamu kufanya Ihiyau. Yaani kusimama usiku kufanya ibada katika misiku ifuatayo:

**MFUNUGO:**

(i) TATU: **Usiku** wa Tarehe 7 kuamkia tarehe 8

**Usiku** wa tarehe 8 kuamkia tarehe 9

**Usiku** wa tarehe 9 kuamkia tarehe 10


(ii) RAMADHANI:

**Usiku** wa kuamkia Idd-El-Fitri

(iii) SHAABAN:

**Usiku** wa tarehe 14 kuamk

**KIAMBATANISHO "D"**



**KIAMBATANISHO "E"**

# MUUNDO WA SEKRETARIETI

